

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**  
**SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA JAMII**  
**IDARA YA KISWAHILI**

**CHANGAMOTO ZA MIKONDO MIPYA YA UTUNZI WA MASHAIRI YA**  
**KISWAHILI: MFANO WA *TUNU YA USHAIRI***

**NA:**

**ONYANCHA JUDY WANGARI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA**  
**MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA**  
**YA UZAMILI YACHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**2015**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

---

SAHIHI

---

TAREHE

ONYANCHA JUDY WANGARI  
C50/27114/2013 (MTAHINIWA)

WASIMAMIZI:

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

---

SAHIHI

---

TAREHE

DKT. EDWIN W.MASINDE  
IDARA YA KISWAHILI  
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

---

SAHIHI

---

TAREHE

DKT. GAKUO J.KARIUKI  
IDARA YA KISWAHILI  
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

**TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Daniel Nyamweya Matundura, mtoto wangu Bryce Nyamweya Onyancha na Mama yangu Annah Nyambeki Onyancha.

**SHUKRANI**

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia fursa na uwezo katika kila hatua ya masomo yangu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nawashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Joseph Gakuo kwa wingi wa busara na hekima iliyonihimiza kuanza, kuendeleza na kuhitimisha kazi hii. Ushauri wenu ulichangia pakubwa katika kufanikisha kazi hii. Mungu awazidishie baraka na hekima.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa kunilea tangu shahada ya kwanza na kunitia moyo kila uchao. Mungu awabariki.

Mpenzi wangu Daniel na mtoto Bryce, natoa shukrani zangu za dhati kwa kunitia moyo kila kuchao na kuvumilia mengi nilipokuwa masomoni. Ahsanteni kwa kugharamia masomo yangu hadi kiwango hiki. Mola awabariki.

Nawahongera pia wenzangu tuliokuwa nao darasani wakiwemo Wanyela, Nasimiyu, Makenge, Kehongo, Ng'etich, Wambua, Winnie, Muthoni, Wamalwa na wote waliotangulia kwa kutufaa na kuhimizana kwa safari hii ya usomi. Nawatakia kila la heri.

## YALIYOMO

Anwani.....	i
Ikirari.....	ii
Shukrani.....	iii
Yaliyomo .....	v
Ufafanuzi wa istilahi muhimu.....	viii
Ikisiri .....	ix
Abstract.....	x

### SURA YA KWANZA : UTANGULIZI

1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Usuli wa mada .....	1
1.2 Suala la utafiti.....	3
1.3 Maswali ya utafiti.....	3
1.4 Malengo ya utafiti .....	3
1.5 Sababu za kuchagua mada .....	4
1.6 Upeo na mipaka .....	5
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	6
1.8 Misingi ya nadharia .....	9
1.9 Mbinu za utafiti .....	12
1.9.1 Muundo wa utafiti .....	12
1.9.2 Mahala pa utafiti.....	12

1.9.3 Sampuli lengwa na mbinu za uteuzi .....	12
1.9.4 Ukusanyaji data .....	13
1.9.5 Uchanganuzi wa data .....	13
1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti .....	13
<b>SURA YA PILI: HISTORIA, MAENDELEO NA MABADILIKO YA USHAIRI</b>	
<b>2.0 Historia, maendeleo na mabadiliko ya ushairi.....</b>	<b>14</b>
<b>2.1 Utangulizi .....</b>	<b>14</b>
<b>2.2 Historia la ushairi.....</b>	<b>15</b>
<b>2.3 Maendeleo yake .....</b>	<b>15</b>
<b>2.4 Urasmi na urasmi mpya katika ushairi wa Kiswahili .....</b>	<b>16</b>
<b>2.5 Kipindi cha waarabu walivyoathiri ushairi wa Kiswahili .....</b>	<b>19</b>
<b>2.6 Kipindi cha ukoloni wa Waingereza .....</b>	<b>20</b>
<b>2.7 Athari ya uhuru katika utunzi .....</b>	<b>22</b>
a) Kipindi cha uhuru na azimio la Arusha .....	23
b) Kipindi cha vita vya Kagera na ugumu wa maisha .....	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
c) Changamoto za Mikondo Mipya Ya Utunzi wa Masha .....	25
<b>2.8 Mikondo na mitindo mipya ya utunzi .....</b>	<b>28</b>
<b>2.9 Dhana ya mgogoro wa ushairi na hali ilivyokuwa.....</b>	<b>29</b>
<b>2.10 Muhtasari .....</b>	<b>33</b>

**SURA YA TATU : MPANGILIO WA MANENO, MISTARI NA UPYA WA VIBWAGIZO**

<b>3.0 Mpangilio wa maneno, mistari na upya wa vibwagizo .....</b>	<b>34</b>
<b>3.1 Utangulizi .....</b>	<b>34</b>
<b>3.2 Mpangilio wa maneno.....</b>	<b>34</b>
<b>3.3 Mpangilio wa mistari.....</b>	<b>40</b>
<b>3.4 Upya wa vibwagizo.....</b>	<b>43</b>
<b>3.5 Muhtasari.....</b>	<b>48</b>

**SURA YA NNE: USHAIRI HURU, USHAIRI PICHA NA USHAIRI ARUDHI**

<b>4.0 Upya katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake na kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi.....</b>	<b>49</b>
<b>4.1 Utangulizi .....</b>	<b>49</b>
<b>4.2 Upya katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake .....</b>	<b>49</b>
<b>4.3 Kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi .....</b>	<b>54</b>
<b>4.4 Muhtasari .....</b>	<b>61</b>

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDELEZO**

<b>5.0 Hitimisho .....</b>	<b>62</b>
<b>5.1 Utangulizi .....</b>	<b>62</b>
<b>5.2 Muhtasari .....</b>	<b>62</b>
<b>5.4 Mapendekezo.....</b>	<b>69</b>
<b>Marejeleo.....</b>	<b>70</b>

Viambatisho .....	70
-------------------	----

### UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

**Changamoto:** Utata unaotokana na kutokuwa na njia moja ya kufasiri ushairi wa Kiswahili.

**Mikondo Mipya:** Ni aina tofauti za tungo katika bahari zilizozoeleka. Kwa mfano, namna mtunzi anavyofuata njia tofauti za kutunga shairi kwa kuzingatia kipengele kimoja.

**Upya:** Kutunga mashairi bila kuzingatia ruwaza na maumbo yaliyozoeleka.

**Ushairi Picha:** Pale ambapo watunzi wanatumia maumbo ya dhana ya kitu wanachokishughulikia kimaudhui.

**Ushairi Arudhi:** Aina ya ushairi unaozingatia kaida za utunzi kama zilivyoielezwa na Amri Abedi

**Ushairi Huru:** Aina ya ushairi usiozingatia arudhi za wanamapoko

**Bahari:** Aina za tungo katika kumbo moja



## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza changamoto zinazotokana na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Malengo ya utafiti yalikuwa kubainisha mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahil, kubainisha mazingira yanayochipuza mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi pamoja na changamoto zake. Ili kufikia malengo haya, utafiti uliongozwa na nadharia ya kimtindo ambayo iliwekewa misingi yake na Coombes (1953) na kuendelezwa na Leech (1969). Coombes anasema kuwa ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani, lazima vipengee vinavyofanya kazi fulani ya fasihi ivutie vizingatiwe. Navyo ni pamoja na matumizi ya taswira, uteuzi wa maneno, urari wa vina na mahadhi ya mashairi. Utafiti huu ulichukua muundo wa kazi kielelezo kimaelezo unaohusu uchunguzi wa kina wa kazi za fasihi kwa njia ya maelezo. Hasa, utafiti wa aina hii huchunguza kazi maalum kindani ili kupata ufahamu wa kina kuhusu kazi nyinginezo zenye sifa sawa. Utafiti ulifanywa maktabani ambapo tahakiki kuhusu utunzi wa mashairi zilishughulikiwa pamoja na yaliyoandikwa kuhusu mada ili kubainisha pengo la utafiti. Sampuli ya mashairi ishirini yaliteuliwa kimakusudi kutokana na mashairi katika *Tunu ya Ushairi*. Data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa mashairi teule. Aidha, mtafiti alidondoa mifano ya sehemu ya mishororo, beti na maneno yaliyoitajika kukidhi mahitaji ya utafiti huu. Data iliyokusanywa ilipangwa kulingana na mpangilo wa mistari, mpangilio wa maneno, upya wa vibwagizo na kujumuishwa pamoja kwa ushairi huru, picha na arudhi. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia ubainishaji wa mikondo mipya, changamoto za mikondo mipya ya utunzi, kuongozwa na mihimili ya nadharia pamoja na maswali na malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji mifano mwafaka katika sura tano. Utafiti huu umepata ya kwamba maendeleo ya utunzi wa ushairi wa Kiswahili katika vipindi mabalimbali vya kihistoria hayana kikomo. Kila kipindi maalum cha kihistoria huathiri ushairi wa Kiswahili kifani na kimaudhui. Hatua hii inadhihirisha kuwa juhudi za kutunga hazina kikomo. Aidha, kuna haja ya kuangalia upya dhana na istilahi zilizozoeleka katika taaluma ya ushairi ili kuafiki kiwango cha maendeleo ya utunzi kwa mujibu wa wakati.

## ABSTRACT

This study investigated the challenges brought about by new stylistic perspectives in Kiswahili poetry. The main objective was to identify new stylistic perspectives in Kiswahili poetry, the settings which contributes to the new patterns of poetic compositions, and the challenges brought about by these new perspectives. In achieving the objectives of the study, the research was guided by the theory of stylistics which was expounded by among others Coombs (1953), Leech (1961). The study has analysed data from an anthology entitled *diwani ya Tunu ya Ushairi*. Inorder to achieve these goals, the study analysed poems from the anthology of *diwani ya Tunu* which apart from focusing on the well known stylistic perspectives, also has got new stylistic modes of style in Kiswahili prosodic poetry. These new styles in Kiswahili poetry have made it necessary to revisit our understanding on how Kiswahili poetry is described and categorized. The research was mainly library based where background reading was done on relevant theories on the criticism and reading of Kiswahili poetry. In addition, information on various issues regarding the styles of poetry was gathered. A sample of Kiswahili poems from *diwani ya Tunu ya Ushairi* was selected using purposive sampling techniques. Using this primary data, the researcher did indepth reading and analysis of the new stylistic attributes under the guidance of the theory of the stylistics. The results were conveyed using a descriptive approach using of examples as per the objectives and organized into five chapters. The research found out that development of poetic composition has no end. Therefore, there is need to review the concepts and terminologies used inorder to be in consonant with current trends.

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 Utangulizi**

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Kufikia hii leo, Ushairi wa Kiswahili umepitia hatua mbalimbali za maendeleo ya utunzi kifani na kimaudhui (Masinde,1992). Kuna mitindo ya awali zaidi yenye kujikita katika kanuni za kiarudhi na kuna mitindo ya baadaye ya washairi kuzivua kanuni hizo .Aina zote mbili za ushairi zimeshuhudia mabadiliko mengi. Mabadiliko haya yanaonyesha kuwa sanaa huchukua mikondo mipya kila uchao lakini bila kujitenga na nduni zake. Upya huu unatufanya tukubali kuwa dhana mbalimbali za ushairi zinafaa kubadilishwa na kupanuliwa kulingana na hali na viwango vya ubunifu katika ushairi (Arege, 2013: vii).

Juhudi za kutunga hazina kikomo.Watunzi wamekuwa wakiibuka na mikondo pamoja na mitindo mipya ya utunzi ili kukidhi mahitaji ya utunzi kwa mujibu wa wakati , mazingira na masuala yanayoshughulikiwa (Masinde, 1992). Ubunifu huu kimaendeleo unautajirisha ushairi wa Kiswahili. Aidha, mikondo mipya ya bahari mbalimbali za mashairi inaonyesha hatua walizozipiga washairi wa Kiswahili. Upya huu unasaidia kuona jinsi washairi walivyotumia ubunifu wao kupanua mawanda ya bahari za ushairi wa Kiswahili. Hivyo, Kuna haja ya kuhakiki ushairi wa Kiswahili upya ili kutoa mchango mufti katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili, hasa, katika kubadilisha mtazamo wetu kuhusu dhana na aina za mashairi katika hali yake ya sasa ya utunzi.

Utunzi wa sasa hauzingatii zile kanuni zilizopendekezwa na akina Amri Abedi (1954). Kipindi cha akina Kezilahabi, ushairi ulipata mwelekeo mpya kutokana na maendeleo na mabadiliko kijamii. Huu upya ni sehemu ya maendeleo ya utunzi wa mashairi yaliyoanza mwaka wa 1968, ambapo kulizuka mashairi yasiyofuata arudhi za kimapokeo. *Tunu ya Ushairi* 2013 ni sehemu ya maendeleo ya watunzi waliokiuka sheria za wanajadi. Katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*, kwa upande wa maneno, kuna mikondo mingi ya bahari ya pindu. Aidha, bahari ya kikwamba nayo imechukua mikondo mbalimbali. Bahari ya ngojera inadhihirisha mikondo mipya iliyotofauti na ile ambayo imezoeleka. Pia, kuna upya mwingi katika namna ya kuuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake mbalimbali. Hali hii inadhihirisha kuwa kulikuwa na haja ya utafiti kufanywa kuhusu hali ya sasa ya ushairi wa Kiswahili.

*Tunu ya Ushairi* imejumuisha pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi (Arege, 2013: vii). Hili linaiongezea diwani hii upekee. Aidha, uwasilishaji jumbe za mashairi umefanywa kwa njia sahili lakini utapata jumbe za mashairi haya kuwa yamesheeni falsafa nzito ya maisha ambayo itakuwa dhahiri tu kwa mwenye kuyatazama kwa jicho la ndani. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kutathmini upya istilahi zilizozoeleka katika utunzi wa mashairi kwa sababu hali ya sasa ya utunzi wa mashairi imezua changamoto.

## 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umechunguza changamoto za mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Mikondo mipya ya utunzi wa mashairi sasa ni sehemu ya historia ndefu ya utunzi wa mashairi ambapo watunzi wamekuwa wakiibuka na mikondo na mitindo mipya ya utunzi. Watunzi wa diwani ya *Tunu ya Ushairi* wametunga mashairi bila kujikita katika mikondo iliyopo tu, bali pia wamezuka na mikondo na mitindo mipya ya utungaji wa mashairi arudhi ambayo hayafuati ruwaza zilizozoeleka. Aidha, diwani hii inajumulisha pamoja mashairi arudhi na yale huru. Hivyo, mkusanyo huu unatoa changamoto kwa wahakiki wa fasihi kutathmini upya maelezo yao kuhusu dhana mbalimbali za ushairi. Hiki kilikuwa kichocheo cha utafiti huu.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a. Je, ni mikondo na mitindo gani mipya iliyotumiwa katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*?
- b. Je, ni mazingira gani yaliyochipuza mikondo na mitindo mipya ya utunzi?
- c. Je, ni changamoto zipi zilizozuka kutokana na mikondo na mitindo hiyo mipya?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

- a. Kubainisha mikondo na mitindo mipya ya utunzi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*.
- b. Kubainisha mazingira yaliyochipuza mikondo na mitindo mipya ya utunzi.
- c. Kueleza changamoto zilizotokana na mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi.

### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Maendeleo ya kutunga mashairi hayana kikomo. Kila uchao watunzi hujaribu kuibuka na mikondo na mitindo mipya ili kukidhi mahitaji ya utunzi wao kwa mujibu wa masuala husika, mazingira na wakati (Masinde 2003). Jambo hili huzua changamoto za ufasiri na utoaji wa maana katika ushairi kadri siku zinaposonga mbele. Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na umepitia mabadiliko mengi kufikia sasa. Kila kipindi cha historia ya jamii kimeuathiri ushairi wa Kiswahili kifani na kimaudhui kwa njia tofauti. Jambo hili huleta maana na dhima mpya katika utunzi. Hatua hii huleta changamoto kuhusu dhana mbalimbali za ushairi.

Kadri asasi nyingine za jamii zinavyobadilika kimaendeleo, utunzi pia hauna budi kubadilika ili kwenda sambamba na kiwango cha urazini wa jamii. Jambo hili pia hubainika katika kiwango cha uhakiki na uhalisia wa mambo (Wafula, 1992). Kwa zaidi ya miongo minne sasa kumekuwa na tetezi kwamba mashairi huru si mashairi (kwa mujibu wa nadharia ya jadi). Hadi sasa, baadhi ya wanajadi wanaoshikilia msimamo mkali kama Sheikh Nabhany bado wanasema kwamba kazi zisizozingatia arudhi si

ushairi na hazina ubunifu wowote. Kauli kama hii haiendani na utunzi katika *Tunu ya Ushairi*. Hivyo, kuna changamoto inayofaa kufanyiwa uchunguzi.

Inatarajiwa kwamba, utafiti huu utawafaidi wakuza mitaala katika kuratibu masomo kulingana na hali ya sasa ya utunzi wa mashairi. Wahakiki, waalimu, wanafunzi na wapenzi wa mashairi wataweza kupata mwongozo mpya na tathmini mpya ya maelezo kuhusu dhana mbalimbali za ushairi kwa kuzingatia hali ya sasa ya utunzi. Hivyo, utafiti huu utasaidia kuondoa utata unaoweza kuzuka kutokana na mikondo mipya ya utunzi.

Utafiti katika kubainisha mikondo mipya ya utunzi wa mashairi katika *Diwani ya Tunu ya Ushairi* haijawahi kufanyiwa utafiti wa kubobea kadri mtafiti ajuavyo.

### **1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu umejikita katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Diwani hii iliteuliwa kimakusudi kwa ambavyo ni mkusanyo wa mashairi ya aina, maudhui na mitindo mbalimbali. Pia, ni diwani ya hivi karibuni katika maendeleo ya utunzi wa mashairi. Aidha, wamezuka washairi wanaotumia mikondo mipya na mitindo ya utungaji inayotoa changamoto kuhusu dhana mbalimbali za ushairi. Vipengele ambavyo vimezingatiwa kuhusiana na mikondo na mitindo mipya ya utunzi ni pamoja na mpangilio wa mistari, mpangilio wa maneno, upya wa vibwagizo, upya katika namna ya kuuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake, kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi. Mashairi kumi na nane yameteuliwa, kila kipengele kilichukua mashairi yanayojitosheleza.

### **1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Tafiti zimefanywa kushughulikia utanzu wa ushairi katika kuhakiki matumizi ya mtindo. Baadhi ya wahakiki walioshughulikia mada hii ni kama vile, Kezilahabi (1974). Alifafanua ushairi kama tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa ufupi ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha. Kutokana na kauli zake mtafiti alichunguza mashairi ya *Tunu ya Ushairi* na kuona changamoto zinazotokana na kauli kama za Kezilahabi kuhusu maana ya ushairi.

Chacha (1987;1992) mtawaliwa, amehakiki ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui akizingatia *Sauti ya Dhiki* na Utenzi wa *Adamu na Hawa*. Chacha ametumia mtazamo wa kimaksi. Utafiti wake ulilenga kuibua maudhui. Hata hivyo, alihakiki vipengele mbalimbali vya kimtindo kwani mtindo hutumiwa kama nyenzo kuu ya kuwasilisha maudhui ya mwandishi. Utafiti wake ulisaidia tafiti huu kwa kuona vile mitindo mbalimbali imetumiwa na watunzi wa mashairi ili kuwasilisha ujumbe wao.

Senkoro (1988) ameshughulikia maudhui na mtindo katika mashairi ya watunzi mbalimbali akiongozwa na nadharia ya Umaksi. Katika utafiti wake, ameshughulikia vipengele mbalimbali vya mtindo na kuonyesha jinsi mtindo unavyosaidia kuwasilisha mawazo ya msanii. Aidha, kupitia utafiti wake anabainisha kuwa mtindo ni namna ambayo msanii huipa kazi ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo inatofautiana na msanii mwingine hata kama jambo linalozungumziwa na wasanii hawa ni moja. Utafiti huu ni tofauti na wake kwa ambavyo utajikita katika kubainisha mikondo



mipya katika diwani teule ya *Tunu ya Ushairi* na pia utafiti huu utajikita katika nadharia ya mwingiliano matini.

Wallah (1988) amejihusisha na suala la urahisishaji wa kueleweka kwa ushairi kwa kutambua jinsi walimu wengi na wanafunzi huogopa ugumu wa ushairi. Amejaribu kutoa kijejezi cha namna jumla ya kuyasoma na kuyachambua mashairi kwa lengo la kuwapa hamasa na motisha wasomi wa mashairi. Utafi ulizingatia baadhi ya vipengele alivyovitaja lakini kwa kuongozwa na malengo mahsusi na nadharia.

Masinde (1992) amehakiki dhamira na mtindo katika mashairi huru ya watunzi kutoka Tanzania. Uhakiki wake ulitumia nadharia ya kimtindo. Katika uhakiki wake, amethibitisha wazo kwamba mtindo hufanya hadhira kuhisi tajriba, mtazamo na mwelekeo wa msanii kuhusu suala analolishughulikia. Utafiti wake ulitusaidia kwa ambavyo ulitupatia mwelekeo kuhusu vipengele na njia za kufanya utafiti. Utafiti wake unatofautiana na huu katika malengo na matini.

Gakuo (1996) ameshughulikia suala la ufasiri na uelewekaji wa tenzi za Kiswahili. Amejikita katika Utenzi wa Vita vya Uhuru wa Shaaban Robert (1945). Utafiti wake ulichunguza fani katika Utenzi wa Vita vya Uhuru. Alijikita katika muktadha wa kihistoria uliochochea mtunzi. Ameongozwa na nadharia ya muundo nan a mtindo kuthibitisha kuwa muktadha na mazingira yanayomzunguka mwandishi pamoja na historia yake ndiyo mihimili na chemchemi ya maudhui na mawasiliano katika ushairi.

Utafiti huu uliboresha utafiti wetu katika kuangalia dhana ya historia na mazingira ya utunzi wa diwani teule.

Njogu na Chimera (1999) wameshughulikia ufasiri wa mashairi ya Kiswahili. Wamezingatia fani na maudhui, wahusika, muundo, mtindo na muktadha na kudhihirisha kuwa shairi lote huwa ni fumbo. Fumbo chambilecho wahenga, hufumbiwa wenye hekima. Ufumbaji kwa mujibu wa Njogu na Chimera una uwezo wa kutatiza mawasiliano baina ya mtunzi na hadhira yake. Wanapendekeza kuwa ufasiri sharti uhusishe udenguaji wa vipengele vya ushairi huku mfasiri akiunda upya ujumbe kulingana na muktadha wa wakati ambamo shairi lilitungwa na baadaye wakati uliopo.

King'ei na Kemoli (2001) wanasema kuwa ushairi ni chombo mwafaka kinachomwezesha mwandishi kuufumbata upana na urefu wa maisha katika maneno teule machache yaliyofinywa kisanaa. Wanaeleza kuwa, kuna hatua mwafaka za kiufasiri ambazo sharti zizingatiwe ili mfasiri aweze kuyadondoa maudhui ya mshairi (uk. 66). Utafiti huu ulisaidia utafiti wetu katika kuona vile waandishi wa mashairi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* walivyowasilisha dhana mbalimbali kwa kufuata mpangilio wa maneno na hata mistari.

Nyanchama (2004) ameshughulikia ufasiri wa ushairi hususan kwa kuzingatia mashairi ya Diwani ya Sauti ya Dhiki (Abdlatif Abdalla). Kulingana na utafiti wake, mtunzi ana uhuru wa kuisuka kazi yake ya ushairi apendavyo. Utafiti wake uliboresha utafiti huu

kwa kutuungazia vile watunzi wa kisasa wametumia ubunifu wao kuzuka na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi. Utafiti wake aidha ulitofautiana na uliofanywa kwani huu ulibainisha mikondo mipya inayotokana na mabadiliko ya kihistoria.

Babusa (2005) ameshughulikia vigezo badalia kuhusu uainishaji wa mashairi ya Kiswahili. Alichambua jinsi mashairi ya Kiswahili yalivyoainishwa katika nyakati mbalimbali na pia alifafanua hali zinazoibusha tanzu mpya za fasihi. Utafiti wake ulipendekeza vigezo vipya vya kuainisha mashairi ya Kiswahili. Alipendekeza kuwa, kuwe na sheria mpya za utunzi zinazojumuisha mashairi ya aina yote pamoja. Ni kwa sababu hii tulichunguza diwani ya *Tunu ya Ushairi* inayojumuisha mashairi yote pamoja na kuibua changamoto za ufasiri wa ushairi wa Kiswahili .

Nabhany amesainisha mashairi ya Kiswahili katika bahari kumi na tatu na kuzitolea ufasiri kila mojawapo. Kazi yake imezingatia tu ushairi arudhi. Kazi hii inakuwa msingi bora wa kuelezea changamoto za mikondo mipya ya utunzi kwa ambavyo haikuzingatiwa katika ushairi jadi.

### **1.8 Misingi Ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kimtindo ambayo iliwekewa misingi yake na Coombes (1953) na kuendelezwa na Leech (1969). Coombes anaeleza kuwa ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani, lazima vipengee vinavyofanya kazi hiyo ivutie vizingatiwe. Vipengee hivyo ni pamoja na matumizi ya taswira, uteuzi wa maneno, urari

wa vina na mahadhi ya mashairi. Wazo kuu la nadharia hii ni kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Jinsi mtunzi anavyotumia lugha ndivyo husaidia kutoa ujumbe kwa wasomaji na hadhira. Hivyo, lugha ndiyo nyenzo kuu ya mawasiliano katika jamii zote za wanadamu (Leech, 1969).

Leech (1969) anasema kuwa kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji. Pia, kazi za kisanaa huchambuliwa kwa kuangalia mitindo ya mwandishi. Alifafanua kwamba:

- a) Maudhui na dhamira hushughulikia falsafa ya mtunzi kuhusu jamii anayoizungumzia.
- b) Muundo wa kazi za kubuni ndio hutumiwa na msanii kutoa ujumbe wake, jinsi alivyounganisha mawazo yake; kuunganisha tukio moja na lingine, mstari mmoja na mwingine, ubeti na ubeti.
- c) Muundo wa kazi hutokana na umbo na mpangilio wa kazi ya fasihi; idadi ya mishororo katika kila ubeti hutupa muundo fulani wa mashairi mbalimbali ya Kiswahili.

Leech anaendelea kusema kuwa lugha ina muundo. Kuna matumizi bayana ambayo husheheni usambamba, urari, tanakali za usemi na ukiukaji ambao huwa na tamathali na upotoshi sarufi. Mtunzi hutumia lugha 'kiajabu' na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya lugha kisanaa. Senkoro (1982) aliyashadidia haya kwa kueleza kuwa utanzu wa ushairi hutumia mpangilio wa lugha mkato. Lugha hiyo

husheheni picha na mapigo mahususi katika kutoa maudhui yake kimuhtasari na aghalabu huyafumba maudhui hayo ndani ya taswira na ishara.

Leech (1981:15) akimrejelea Aristotle na Plato anaeleza kuwa yaliyomo na jinsi yanavyowasilishwa ni kama mwili na roho. Hii ina maana ya kuwa maudhui na namna yalivyowasilishwa ni mambo mawili yanayotegemeana na kuathiriana .Aidha, anaeleza kuwa katika matini tunaweza kuchunguza muundo kwa kina ili kuona ni maneno au sauti zipi zilizopendelewa kuliko zingine.

Wanamtindo husisitiza umuhimu wa lugha kama chombo kitekelezi kinachosaidia katika kuelewa maudhui yaliyokusudiwa.Wanaeleza kuwa vipengele vya kiisimu hutumika kueleza jinsi lugha hutumika. Kutokana na mtindo wa kazi hiyo, huwezi kubadili neno au kauli bila kuubadili mtindo mzima wa kazi ya fasihi.Nadharia hii husisitiza uwiano kati ya ujumbe na lugha kwa sababu lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwani hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi.

Nadharia hii iliongoza utafiti huu kwa kumsaidia mtafiti kuchunguza maumbo mbalimbali ya mashairi katika kutoa ujumbe. Pia, ilisaidia kuangalia mikondo iliyofuatwa na watunzi katika kuyavuma mashairi teule. Kwa kufanya hivyo, mtafiti aliweza kubainisha mikondo ambayo haikuzoeleka, hivyo kusaidia kubainisha changamoto zinazotokana na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi.

## **1.9 Mbinu za Utafiti**

### **1.9.1 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ulichukua muundo wa kazi kielelezo kimaeezo. Kazi kielelezo inahusu uchunguzi wa kina kwa njia ya kimaeezo kwa ujumla kuhusu kazi maalum. Utafiti wa aina hii huchunguza kazi maalum kindani, ili kupata ufahamu wa kina kuhusu kazi nyinginezo zenye sifa sawa. Katika utafiti huu, kulitolewa maelezo kuhusu ubainishaji wa mikondo mipya ya utunzi, changamoto zinazotokana na mikondo hiyo mipya na kubainisha mazingira yaliyochipuza mikondo mipya ya utunzi.

### **1.9.2 Mahala pa Utafiti**

Utafiti ulifanywa maktabani ambapo tahakiki kuhusu utunzi wa mshairi ulishughulikiwa ili kuimarisha mada ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia pamoja na mbinu za kuzingatia kuhusiana na utafiti huu. Vilevile, data iliyohitajika ilikusanywa maktabani kwa kuzingatia diwani teule ya *Tunu ya Ushairi*.

### **1.9.3 Sampuli Lengwa na Mbinu za Uteuzi**

Sampuli lengwa ni mashairi ya *Tunu ya Ushairi*. Data iliyohitajika ilitokana na mashairi ambayo yaliteuliwa kwa kuzingatia mbinu kusudio. Uteuzi sampuli kimakusudi uliegemezwa kwa kile kinachomwongoza mtafiti, yaani sababu fulani maalum za kitafiti na kiuchunguzi alizonazo. Mashairi ishirini kutoka diwani ya *Tunu ya Ushairi* yaliteuliwa kutathmini na kukadiria kiwango cha mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Kila kipengele kilijumuisha mashairi manne.

#### **1.9.4 Ukusanyaji Data**

Mbinu kuu ya ukusanyaji data ilikuwa usomaji wa kina wa mashairi teule. Katika kufanya hivyo, mtafiti alidondoa mifano ya sehemu, mishororo, beti na maneno kama mifano ya data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu.

#### **1.9.5 Uchanganuzi wa Data**

Data ambayo ilikusanywa ilipangwa kulingana na vipengele vifuatavyo: Mpangilio wa mistari, mpangilio wa maneno, upya wa vibwagizo, upya katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi na kujumuishwa pamoja kwa ushairi huru, picha na ushairi arudhi. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia ubainishaji wa mikondo mipya, changamoto za mikondo mipya ya utunzi kwa kuongozwa na maswali, malengo pamoja na mihimili ya nadharia.

#### **1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti**

Uwasilishaji wa matokeo ulikuwa wa njia ya maelezo pamoja na utoaji wa mifano mwafaka ya mashairi ambayo yana data iliyotimiza malengo ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 HISTORIA, MAENDELEO NA MABADILIKO YA USHAIRI.**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii iliangalia historia, maendeleo na mabadiliko ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kubainisha ya kwamba juhudi za kutunga hazina kikomo. Kila uchao watunzi wamekuwa wakiibuka na mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Jambo hili limezua changamoto na kuathiri maana na ufasiri wa ushairi wa Kiswahili. Vilevile, katika sura hii tumebainisha kwamba historia la kazi yoyote ya kisanaa ni mazingira maalum ya historia ya jamii kwa mujibu wa wakati. Kwa njia hii, tumeweza kubainisha maendeleo ya ushairi, mazingira na historia la mitindo mipya ya utunzi. Aidha, tumeweza kuangazia changamoto zinazotokana na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

Maelezo katika sura hii yameongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya mtindo. Mhimili huu unasema kwamba, maudhui na dhamira hushughulikia falsafa ya mtunzi kuhusu jamii anayoizungumzia kwa mujibu wa wakati na fani anayoitumia. Hivyo, humwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa njia ifaayo. Sura hii imetuwekea msingi wa kuelewa historia la mikondo na mitindo ya utunzi katika muktadha wa maendeleo ya utunzi wa ushairi wa Kiswahili.



## **2.2 Chimbuko la Ushairi**

Ushairi wa Kiswahili una umri sawa na waswahili wenyewe. Unapatikana katika historia la mswahili, lugha yao na utamaduni wao. Ulianza wakati binadamu alibuni lugha na kuwa kiumbe razini: Alianza kuyaelewa mazingira yake, kutoa mchango wake ili kuyakabili mazingira hayo, kuweza kuyabadilisha, kushirikiana na wenzake kwa kuwasiliana, kuweza kujielewa na kuelewa mazingira yake, kufanya kazi na kuzalisha mali.

Asili yake ni nyimbo zilizokuwa zikiimbwa katika sherehe na ngoma mbalimbali zikiwemo harusi, kilimo, uwindaji, unyago, jando, pungwa, wakati wa kufanya kazi ya ushirikiano, kubembeleza watoto na hata wakati wa majonzi. Kulikuwa na mashindano hadharani. Manju walijibizana kishairi na kuvishana vilemba. Aidha, mashairi yalitungwa ili kuelezea visa vya kishujaa kama vile utenzi wa Liyongo. Pia, mashairi yalitungwa kuelezea hisia za jamii, matamano na matarajio, thamani za jamii, historia na mashujaa n.k .Ushairi wa kale haukuwa ukihifadhiwa kimaandishi. Ulichukua umbo la kimasimulizi. Waswahili hawakuwa na hati za kuhifadhia. Kulikuwa na ugumu wa kusoma wala kuandika. Kipawa cha kutunga kilitokana na mungu (Harries, 1962)

## **2.3 Maendeleo yake**

Katika kuangalia maumbo ya mashairi, mwanzoni kabisa hayakufuata utaratibu maalum wa kuyaimba. Mashairi hayo yalikuwa hayana vina na mizani. Kila uchao manju na malenga walijitahidi kuziendeleza mbele nyimbo hizo. Baadaye, walianza kutumia

utaratibu maalumu wa kuziimba wa kutumia urari na vina vya mwisho pekee. Katika hatua hiyo, kulikuwa bado kuzinduliwa kwa ulinganifu wa vina vya kati na ulinganifu wamizani (Athmani, 1728).

Maendeleo ya baadaye yalileta nyimbo za mistari mingi na mizani pia. Nyimbo hizi zilianza kulinganisha idadi ya mizani katika mistari yake lakini zikawa bado hazina vina vya kati. Nyimbo nyingi za aina hii zilikuwa na madhumuni ya kutumbuiza ndipo kulitokea utanzu wa tumbuizo.

Baada ya hapo, nyimbo zilianza kugawanywa katika beti zenye mizani zilizokuwa fupifupi. Kila mstari ukawa na mizani sawa na mstari mwingine. Hata hivyo, bado nyimbo hazikuwa zimepata urari wa vina vya kati. Baadaye, ikafikiwa hatua nyingine ambapo kila ubeti kuwa na urari wa vina vya kati. Nyingi ya nyimbo katika utanzu huu ni ni zile za tathlitha na tathnia. Kisha, utungaji ulishamiri uswahilini na kukaibuka miundo mbalimbali ya kishazi. Umbo lililoelekea kupendeka zaidi mpaka leo hii ni la mistari minne kila ubeti na mizani 16 katika kila mstari (Knappert ,1979). Malenga walizidi kuupenda na kutaka kuutumia kuelezea matukio makubwa katika jamii, historia, ushujaa wa watu wao miongoni mwa mengine. hapo ndipo utanzu wa utenzi ulipozuka.

#### **2.4 Urasmi na Urasmi Mpya Katika Ushairi wa Kiswahili**

Urasimi ni kipindi maalum katika historia ya jamii ambapo misingi ya utunzi hubainishwa na kukubalika kuwa vipimo vya kazi zinazofaa kutungwa na wasanii. Katika

fasihi ya Kiswahili, kipindi hiki kilikuwepo katika karne ya 18 na 19 hasa tukiangalia mashairi na tenzi zilizotungwa wakati huo. Kwa mfano; inkishafi,kiama, mwanakupona miongoni mwa zingine.Kazi hizo zilisisitiza maumbo maalum, lugha teule pamoja na ujumbe mahususi wa kushughulikia (Mayoka, 1993).

Sura za kimuundo za kipindi hiki zilikuwa kwamba mashairi yawe na utangulizi. Hapa mtunzi alianza kwa kuomba dua kwa mwenyezi mungu ili ampe uwezo wa kutunga utungo unaostahiki. Kisha,mtunzi alitaja au kueleza lengo la kazi yake. Alafu, alikita katika masimulizi ya kina yaliyoibua kwa ufasaha ujumbe mkuu, dhamira pamoja na mafunzo ya mtunzi. Katika hatua ya mwisho, mtunzi alihitimisha utungo wake kwa kuomba msamaha kwa kasoro au makosa yoyote ambayo yalienda yakatokea katika utunzi wake (Mayoka, 1993)

Pia, alitaja nasaba yake na kumshukuru mungu kwa kumwezesha kukamilisha utungo wake. Aidha, alitoa ujumbe mahususi kwa wasomaji wake.

Upo uwiano mkubwa baina ya kanuni za ushairi wa kimapokeo wa Kiswahili na ule wa Kirumi na Kigiriki uliotawala matamko mengi ya wanafalsafa wa mwanzo, akina Socrates, Plato na Aristotle (Senkoro, 1987).Katika kipindi hiki, kulikuwepo na kanuni zifuatazo; Umuhimu wa vina na mizani katika ushairi,Ulazima wa kuwa na muundo mahususi, suala la kupagawa kunakotokana na nguvu za Mwenyezi Mungu,lugha teule,suala la mwigu pamoja na hadhira

Kwa mujibu wa vigezo hivi, tunapata kuwa hadi sasa, imani za “sheria” za kiurasmu katika ushairi wa Kiswahili bado zinashikiliwa na kusisitizwa na Wanajadi au Wanamapokeo. Hii ndiyo chanzo cha mgogoro katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili. Kulikuwa na kuenzi kwa sheria na kanuni katika utunzi, kilichowafanya Wanajadi kudai kwamba ni uti wa mgongo wa shairi, licha ya kuwa ndilo shairi lenyewe. Katika mashairi mengi na tenzi nyingi za kiurasmu, kuna uzingatiaji wa arudhi na miundo ambapo kazi zilizohusika zilikuwa na mwanzo ulio na dibaji inayomhusisha msanii na Mungu. Sehemu ya kati ya kazi hizo ni kiini cha mtunzi. Kisha, mwisho ulikariri juu ya sifa za Mungu zenye dua na shukurani. Suala la lugha teule lilijitokeza kuwa kigezo muhimu cha ushairi wa kirasimi. Kwenye ushairi wa kirasimi wa awali wa Kiswahili, lugha ya Baraza ya lahaja ya Kingozi iliyokuwa ya serikali ya Pate ilitumiwa.

Kipindi cha urasmi mpya wa ushairi wa Kiswahili, washairi kama vile Shaaban ,Abed, Mnyampala miongoni mwa wengine wanaonyesha kufuata kanuni za ushairi wa awali. Kazi zao zinabainisha arudhi pamoja na kutawaliwa na lugha teule. Hili linadhihirisha kuwa kipindi cha urasmi kulikuwa na ushairi wa kiukoo. Wakati ambapo ushairi wa Kiswahili ulipoanza kuachana na koo za kishairi, urasmi mkongwe ulianza kufifia. Ule urasmi-mpya wa kina Shaaban na wengine uliingia. Washairi hawa wa urasmi mpya walipofariki, urasmi huo mpya nao ulianza kufifia (Senkoro, 1987).

## **2.5 Kipindi cha Waarabu walivyoathiri ushairi wa Kiswahili**

Waarabu ndiyo wageni wa mwanzo kuja katika upwa wa Afrika Mashariki. Hawa walikuja na kuanza kufanya biashara na wenyeji wa upwa huo ikiwamo biashara ya watumwa. Waarabu pia walileta dini ya Kiislamu ambayo ilianza kuwa maarufu na watu wakaacha dini yao ya jadi. Aidha, Waarabu walileta hati zao za Kiarabu. Dini hii na hati za kiarabu, zilikuwa na athari kubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Hati za Kiarabu zilianza kutumika katika kuhifadhi ushairi wa Kiswahili.

Kwa vile watunzi wengi wa mashairi walikuwa wamebadilisha dini na kuwa waisilamu, hata maudhui ya mashairi yao yalisawiri dini hii. Vilevile, kutokana na hilo hata aya za Korani na dua za Kiislamu zilianza kuingizwa katika ushairi wa Kiswahili. Pia, muundo wa mashairi ya Kiarabu ulianza kutumika katika mashairi ya Kiswahili. Hapa ndipo ushairi wenye urari wa vina na mizani ulipoingia kutokana na kuisitiza uzingatiaji wa urari wa vina na mizani katika utunzi. Kadhalika, istilahi za utunzi wa mashairi pia zililetwa kama vile beti, mishororo na majina ya bahari za ushairi kama vile tarbia, tathlitha miongoni mwa mengine. Kuna tanzu mbili za ushairi wa Kiswahili zilizotokana na asili ya kiarabu; ule wa takhmisa na hamziya (Senkoro, 1987).

Katika takhmisa kulikuwa na watunzi wawili. Mashairi wa kwanza alitunga mistari miwili ya mwisho. Yule wa pili alitunga mistari mitatu ya kwanza lakini kwa kutumia kina cha mtari wa kwanza kati ya ile miwili ya mtunzi wa kwanza. Ilihitajika kwamba, ile

mistari inayoongezwa isiharibu maana iliyokusudiwa. Na iwapo ile mitatu itaondolewa, ile miwili ibaki na maana yake ile ya mwanzo. Utungo wa Hamziya ulikuwa na mistari miwili miwili ambayo haikugawanyiki katika vipande. Silabi ya mwisho wa mstari wa kwanza si lazima iwe sawa na silabi ya mwisho ya mstari wa pili. Lakini silabi zake za mwisho katika mistari yote ya mwisho sharti zingekuwa na urari(Abedi, 1954).

## **2.6 Kipindi cha Ukoloni wa Waingereza**

Ukoloni wa Waingereza ulianza baada ya Wajerumani kushindwa katika vita vikuu ya kwanza dunia na hivyo makoloni yake kugawanywa miongoni mwa mataifa yaliyoshinda vita. Moja ya mataifa hayo ni Uingereza. Katika kipindi hiki shule ziliendelea kutoa elimu ya ushairi na pia magazeti yaliongezeka. Kulikuwa na magazeti kama vile *Msimulizi*, *Pwani na Bara* na *mambo leo*. Aidha, katika kipindi hiki palishuhudiwa pia kupiga hatua katika taaluma ya uchapaji wa vitabu. Ushairi wa Kiswahili ulipiga hatua kubwa katika kipindi hiki na ndipo sheria na kanuni za utunzi wa ushairi zilitungwa na Amri Abedi mnamo mwaka 1954 katika kitabu chake *Sheria za Kutunga Mashairi* na *Diwani ya Amri*. Katika kitabu hicho, Abedi anaona kuwa kuenea kwa vitabu na magazeti kumewafanya watu wengi watake kutunga mashairi.

Abedi anaeleza kuwa mashairi mengi yaliyotungwa, yalitungwa bila ujuzi wa kutosha, nayo yalielekea kupunguza thamani ya mashairi ya Kiswahili mbele ya mashairi ya lugha nyingine. Aliona ni vema kueleza kanuni za kutunga mashairi ili kuwarejesha watungaji katika mipaka iliyotakiwa. Abedi alifasili shairi au utenzi kuwa ni wimbo. Kama shairi

halikuimbika halikuwa na umuhimu wowote. Pia alieleza kuwa utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, ambao mara nyingi hukosa vina vya kati katika mstari, bali kila ubeti ulipaswa kuwa na vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho katika kila ubeti ambao uliendelea na kina cha namna moja kinachoitwa *bahari*. Aliendelea kusema kuwa utenzi wa mizani nane uliimbika vizuri. Lakini pia iliwezekana kuwa na tenzi zenye mizani kumi na moja kama vile *al-Inkishafi* na pia kulikuwa na zenye mizani sita.

Andiko hilo la Abedi lilibainisha mambo makuu manne ambayo ni muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Mambo hayo ni vina, mizani, kituo na utoshelevu. Abedi anadai kuwa shairi la Kiswahili halina budi kuwa na urari wa vina na mizani. Anasisitiza kwamba vina na mizani ndiyo uti wa mgongo wa shairi lolote lile la Kiswahili. Zaidi ya urari wa vina na mizani, anasisitiza umuhimu wa kituo ambacho anakieleza kuwa ni mstari wa mwisho wa kila ubeti. Huo huwa ama ni kiini cha habari (haubadiliki) ama kimalizio (hubadilika). Kituo kinapokuwa kimalizio, basi kinabadilikabadilika ambapo kina cha mwisho huenda kati, mwisho na kadhalika. Jambo la mwisho analolisisitiza ni utoshelevu ambapo anadai kwamba kila ubeti ujitosheleze kadri iwezekanavyo: yaani uwe na maana kamili na maana hiyo isingoje kukamilishwa na ubeti mwingine unaofuata.

Mambo mengine anayoeleza Abedi ni kwamba, kazi iliyongumu katika kutunga shairi hasa kwa anayejifunza ni kupata vina vilivyo sawa na vizuri, vitoavyo maana, vyenye maneno mbalimbali. Kina cha “ni” ni chepesi zaidi. Kupata vina kwa haraka inabidi

ujizoeze kusoma sana mashairi mazuri ya watu mbalimbali. Watunzi wa mashairi wasiige ovyo bali wakuze vipaji vyao kwa kuwa na shauku ya kutunga na kusoma mashairi ya wengine. Tunga iwapo haja; tunga shairi kwa jambo linalokusukuma sana ndipo mashairi yatapenya moyo, la sivyoyatakuwa chapwa. Tumia lugha nyepesi ukizungumzia mambo ya kawaida. Usitunge mambo ya kihuni bali yale yawafaayo, yaelimishayo, yafikirishayo na pia yafurahishayo watu. Tumia lugha ya kizamani unapotaka kuzungumzia shairi zito la fikra, tumia methali katika kituo na pia dokeza na mafumbo. Lugha inayotumiwa na wanawake pia ni safi; huchapusha shairi. Haya yote ni mapendekezo ya Abedi.

## **2.7 Athari ya Uhuru katika Utunzi**

Katika wakati wote wa utawala wa wakoloni, Waswahili hawakuwa wametulia, bali waliendeleza mapambano yao ya kuleta ukombozi na kurudisha heshima yao. Wapo waliotumia njia za amani na wapo waliotumia kama baadhi ya mbinu hizo. Penye nia huwa njia, hatimaye kuanzia miaka ya 1960 nchi za Afrika Mashariki zikaanza kujipatia uhuru.

Tanganyika ilipata uhuru wake 1961, Kenya 1962, Zanzibar 1964 na Uganda 1964. Katika kuelezea historia ya Kiswahili baada ya uhuru, tumegawa kipindi hicho katika vipindi kadhaa vidogovidogo.



**a) Kipindi cha Uhuru na Azimio la Arusha**

Kipindi hiki kinaanza mwaka wa 1961 na kuishia mwaka wa 1970. Katika kipindi hiki mashairi mengi yalikuwa ya kushangilia uhuru na kuwapongeza wapigania uhuru kwa kazi yao nzuri. Mashairi ya aina hiyo yanaonekana katika mashairi marefu kama vile; *Utenzi wa uhuru wa Tanganyika (1967)* ulioandikwa na Mwinyihatibu Mohamed Amiri; *Utenzi wa Jamuhuri ya Tanganyika (1967)* ulioandikwa na Ramadhani Mwaruka; *Utenzi wa Uhuru wa Kenya (1972)* ulioandikwa na Salim A. kibao na *Utenzi wa jamuhuri ya Zanzibar*.

Mwaka wa 1967 Azimio la Arusha lililoambatana na siasa ya ujamaa na kujitegemea lilitangazwa na hivyo kuleta sura mpya ya ushairi wa Kiswahili. Mashairi ya kijamaa-yaliyosifia Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa na kujitegemea yaliibuka. Miongoni mwa mashairi hayo ni *Mashairi ya Azimio la Arusha (1971)* yaliyohaririwa na Grant Kamenju na Farouk Topan. Pia fani/mtindo mpya wa ushairi wa kimajibizano ulianzishwa ambao ulipewa jina ngonjera. Mfano mzuri wa ushairi huo wa kimajibizano unaonekana katika Ngonjera za UKUTA za Mnyampala 1970.

Ngonjera hizi zilitumiwa sana na wanasiasa kueneza siasa ya ujamaa na kujitegemea. Hata hivyo, Mbaga katika makala yake iitwayo “Ngonjera: Historia yake Simulizi hadi Andishi” iliyopo kwenye jarida la Kiswahili anaeleza kuwa fani hii ya ngonjera imekuwepo katika jamii mbalimbali hata kabla ya wakati huo. Dai hili la Mbaga linathibitisha tu kuwa ushairi andishi wa Kiswahili unachimbuka katika ushairi simulizi

wa Kibantu uliokuwepo tangu kale. Hoja yetu hapa ni kuwa, hata kama ngonjera simulizi zimekuwepo kwa muda mrefu ngonjera andishi zilianza kuonekana katika wakati huu. Ushairi mwingi wa wakati huu ulikuwa wa kikasuku. Kasuku ni ndege mwenye tabia ya kuiga kila sauti anayoisikia bila kujua maana yake na madhara yake. Mashairi hayo yalisifia kila jambo lililosemwa na wanasisia bila kudhihirisha kufaa kwake.

#### **b) Kipindi Cha Vita Vya Kagera Na Ugumu Wa Maisha**

Katika kipindi hiki palianza kuibuka hali ya kukata tamaa miongoni mwa watu kutokana na matamano na matarajio yao baada ya uhuru kutotimizwa. Baada ya uhuru, watu waliamini kwamba maisha yao yangukuwa mazuri zaidi na kungekuwa na neema zaidi lakini hali haikuwa hivyo. Hapa ndipo ulipoibuka ushairi wa kihakiki ambao uliikosa jamii.

Ushairi wa kipindi hicho ulionesha hali halisi ya jamii katika nyanja mbalimbali kama vile hali ya kisiasa, uongozi mbaya, ukiritimba, kujilimbikizia mali, uhujumu uchumi na kadhalika. Washairi pia walianza kutathmini upya kuhusu Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa na kujitegemea . Hapa ndipo palipoibuka mashairi kama *Miaka Kumi Baada ya Azimio la Arusha* (1977) yaliyohaririwa na Abdilatif Abdalla. Mashairi hayo yanaonyesha jinsi hali ya kiuchumi na kijamii ilivyokuwa mbaya. Mathalani, yalionyesha jinsi wananchi walivyokuwa wanapata tabu kupata mahitaji muhimu. Mashairi mengine ya mkondo huu ni ya Kezilahabi (1974) *Kichomi* na (1988) *Karibu Ndani*; ya Kahigi na

Mulokozi (1976) *Malenga wa Bara* na ya Mohamed Seif Khatib (1988) *Fungate ya Uhuru*.

Watunzi hawa walipendekeza mbinu mbalimbali za kuondokana na matatizo hayo ikiwa ni pamoja na kuwahimiza wananchi kuungana ili kutatua matatizo yao na kuchukua hatua. Aidha, yalipendekeza pia viongozi kuwajibika ama kuwajibishwa ili kuepusha matatizo zaidi. Hali hiyo inaonekana katika mashairi ya *Fungate ya Uhuru* (1988) na ya Mochiwa (1988) *Mvumilivu Hula Mbivu*. Mochiwa anasisitiza kwamba huu si wakati wa wananchi kuwavumilia viongozi wasiofaa maana mvumilivu hula mbivu. Kwa ujumla, watunzi hawa walitaka ujenzi wa jamii mpya ambayo itakuwa na haki, uchumi imara, jamii iliyojikomboa kiutamaduni, yenye watu wazalendo, yenye umoja, usawa na utu na ambayo ina viongozi bora. Kwa mfano, Kezilahabi katika kitabu cha *Karibu Ndani* katika shairi “Chai ya Jioni” anabainisha maovu haya ya viongozi.

Mshairi anaonyesha jinsi viongozi wanavyojisahau wakiwa madarakani. Anawakumbusha kuwa wanapona mambo yanaenda wajue na muda wa uongozi wao unaisha pia.

Hivyo, anadai kuwa ni vema wahakikishe kuwa kabla hawajaondoka madarakani wanafanya mambo yanayokubalika katika jamii. Mashairi mengine ya mkondo huu katika diwani hii ni pamoja na shairi la pili kitabuni “Mkesho,” la tatu “Matumaini” na mengineyo mengi. Katika shairi la “Mkesho” mwandishi anabainisha kwamba wakati

watu wanateseka wakisubiri maendeleo viongozi wanaishi maisha ya kifahari; katika shairi la “Matumaini” mwandishi anabainisha jinsi Waafrika waliokuwa na matumaini makubwa wakati nchi zao zilipata uhuru kuwa viongozi wa Kiafrika watawaletea maendeleo, walivyokata tamaa na kukosa matumaini kabisa. Kwa ujumla, mshairi huyu amesawiri sana hali ya kukata tamaa iliyokuwepo wakati huo.

Hata hivyo, izingatiwe kuwa mashairi haya yanaweza kuchambuliwa kwa namna nyingine na kupewa dhamira nyingine. Kwa mfano, Senkoro anaona kuwa shairi la “Chai ya Jioni” linahusu mapenzi na wala si siasa kama tunavyodai hapa. Mtazamo huu wa Senkoro unatuonyesha kuwa kazi ya fasihi huweza kuhakikiwa kwa namna tofautitofauti na kubainika kuwa na dhamira tofautitofauti kulingana na mhakiki. Kwa upande wa mashairi yanayohimiza ukombozi wa kiutamaduni yanaonekana katika vitabu mbalimbali. Kwa mfano, Diwani ya Akilimali (1963) cha Akilimali Snow-White na *Ngonjera za Ukuta* cha Mathias Mnyampala (1970) mashairi ya aina hii ni mengi sana.

Diwani ya Akilimali, shairi la “Kila Mdharau Chake” msanii anasisitiza watu kudhamini vya kwao, ikiwa ni pamoja na utamaduni wao. Aidha, *Ngonjera za Ukuta* msanii mtunzi ameweka safu maalumu yenye mashairi yanayohusu elimu na utamaduni. Mtunzi kwenye safu hii ametunga mashairi mengi ambayo yanahimiza ukombozi wa kiutamaduni. Miongoni mwa mashairi hayo ni pamoja na “ Utamaduni Kitu Gani ” na “ Kiingereza Lugha Nzuri?”. Shairi la “Utamaduni Kitu Gani” msanii anaielimisha jamii juu ya dhana nzima ya utamaduni wa Kiafrika na kuwataka wauheshimu utamaduni wao maana ni

bora. Shairi la “Kiingereza Lugha Nzuri” msanii anahoji uzuri wa lugha ya Kiingereza. Katika shairi hilo, anawakejeli wanajamii wanaoona kwamba kujua Kiingereza ndiyo usomi na ujuzi wa mambo na kuwakumbusha kuwa Kiswahili ni lugha inayojitosheleza na lugha ya usomi pia. Kwa kusema hivyo, msanii alikusudia kuikomboa jamii kutokana na ukoloni wa kiutamaduni.

### **c) Changamoto za Mikondo Mipya**

Mabadiliko ambayo ushairi wa Kiswahili umepitia umepelekea kuibuka kwa changamoto mbalimbali kwa wasomi wa fasihi ya Kiswahili. Mikondo mipya ya utunzi wa mashairi sasa ni sehemu ya historia ndefu ya utunzi wa mashairi ambapo watunzi wamekuwa wakiibuka na mikondo na mitindo mipya ya utunzi. Watunzi wa diwani ya *Tunu ya Ushairi* wametunga mashairi bila kujikita katika mikondo iliyopo tu, bali pia wamezuka na mikondo na mitindo mipya ya utungaji wa mashairi arudhi ambayo hayafuati ruwaza zilizozoeleka. Aidha, diwani hii inajumulisha pamoja mashairi arudhi na yale huru. Hivyo, mkusanyo huu unatoa changamoto kwa wahakiki wa fasihi kutathmini upya maelezo yao kuhusu dhana mbalimbali za ushairi. Hiki kilikuwa kichocheo cha utafiti huu. kuwa upya katika uwasilishaji wa mpangilio wa mistari, maneno na upwa wa vibwagizo katika *Tunu ya Ushairi* unazua changamoto kwa wahakiki wa mashairi katika kufasili istilahi zilizozoeleka. kwamba, kuna ruwaza tofauti na zile ruwaza za awali za kutunga mashairi kwa kuzingatia vipengele vilivyotajwa.

Kujumuishwa pamoja mashairi mbalimbali, kunasaidia kuondoa mipaka iliyokuwepo awali iliyotenganisha ushairi arudhi na ushairi huru. Upya katika kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake pia ni hatua inayozua changamoto katika namna ya kufasili dhana mbalimbali ikiwemo dhana ya ngojera. Kwa hivyo, changamoto zinatokana na ufasili wa dhana na maana za kishairi katika muktadha wa awali wa hali zilizozoeleka.

## **2.8 Mikondo na Mitindo Mipya ya Utunzi**

Sehemu hii imeangalia kuibuka kwa mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Katika kipindi hiki palishuhudiwa mabadiliko ya kifani yaliyotokana na kuibuka kwa ushairi wa kisasa. Mabadiliko haya ndiyo yanayoitwa majaribio katika ushairi. Majaribio yamekuwapo katika tanzu mbalimbali za fasihi pia. Mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili yalianza tangu mwishoni mwa miaka ya 1960 lakini yakashika kasi sana na kuwa bayana zaidi katika kipindi cha miaka ya 1970. Na hayo ndio mazingira yaliyochipuza aina mpya ya utunzi. Kufikia miaka ya 1970 kulikuwa na majaribio ya wazi ya kutunga mashairi yasiyozingatia kanuni za awali zilizopendekezwa na akina Amri Abedi. Mashairi haya yanaonekana kwa wingi katika kazi za E. Kezilahabi, K. K. Kahigi na M. M. Mulokozi, D.P.B Massamba, S.A Mohamed, M.S. Khatibu, Mochiwa, Kithaka wa Mberia, F.E.M.K. Senkoro na wengineo.

Majaribio haya yalipingwa na washairi wengine wa kijadi na kupelekea kuibuka kwa mgogoro katika ushairi. Wanajadi wanaojulikana zaidi ni Andanenga, M. Mnyampala, J. Mayoka, S. Robert, Amri Abedi, Said Karama, Abdilatif Abdala, Ahmad Nassir,

Chiraghdin, Kandoro, Mayoka na Nabany. Wanajadi wakayaita mashairi ya kisasa kuwa masivina, mapingiti na majina mengine yasiyofaa wakiwa katika harakati za kuyadhalilisha. Mgogoro huu unafafanuliwa kwa kina na Jumanne Mayoka katika kitabu chake; *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*.

## **2.9 Dhana ya Mgogoro wa Ushairi na Hali Iliyokuwa**

Mgogoro ni hali ya kutokukubaliana au hali ya mvutano baina ya watu wawili au makundi mawili ya watu. Tunapozungumzia mgogoro wa ushairi, ni kutokukubaliana na mvutano baina ya makundi mawili ya washairi na wanafasihi juu ya dhana ya ushairi wa Kiswahili. Makundi haya yaliyokuwa yanakinzana ni kundi la washairi wakongwe, wanamapokeo, na kundi la washairi wapya, wanausasa. Wanamapokeo hujulikana kama wana ujadi na wanausasa hutambulika kama wanamamboleo. Makundi haya mawili yalikusisha washairi wenyewe pamoja na wataalamu wengine wa fasihi ambao si washairi.

Kila kundi lilikuwa na mtazamo wake juu ya dhana ya ushairi na kuamini kuwa mtazamo wao ni bora zaidi na hivyo kutokuwa tayari kukubali kubadilika au kuukubali mtazamo wa kundi lingine. Mgogoro huu ulijibainisha kwenye midahalo, vyombo vya habari, mashairi na hata katika maandiko mengine yasiyokuwa ya kishairi. Kwa mfano, midahalo iliyofanyika kwenye makongamano mbalimbali mikinzano baina ya makundi hayo ilibainika waziwazi. Mingi ya midahalo hiyo iliitishwa na idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia kupitia vyombo vya habari mikinzano hiyo

ilijibainisha ambapo washairi hawa walijibizana juu ya dhana hasa ya ushairi wa Kiswahili.

Mashairi mengi yaliyoandikwa kwa vyombo vya habari vya wakati huo na hasa magazeti yalikuwa na majibizano baina ya wafuasi wa makundi haya. Aidha, majibizano hayo yalionekana hata katika mashairi waliyoyatunga vitabuni. Mfano mzuri wa mashairi ya aina hiyo yanabainika katika Diwani ya Andanenga, Diwani ya Karibu Ndani, Diwani ya Amri miongoni mwa nyingi nyinginezo. Diwani ya Karibu Ndani ina shairi linalobeba anwani ya diwani hiyo litwalo “Karibu Ndani” ambalo linasawiri mgogoro huo wa ushairi.

Kezilahabi anawaeleza katika shairi la Karibu Ndani kuwa ,wanamapokeo kuwa ushairi wao unafikia mwisho na aina mpya ya ushairi, ushairi wa kisasa, inashika hatamu. Hili linabainika katika ubeti wa kwanza anaposema,”Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lalasalama katika mionzi hafifu, ya jua machweoni na mahadhi yagaagaa, juu ya bahari ya utenzi yameshindwa chini kuzama, kwenye kina cha urazini. Nao wahenga vibandani, nje tena hawatoki hakuna tena ngoma, ya kugeeana kani na ushairi umehama, umerudi peponi lakini majani makavu, sasa hayatingishiki nayo madirisha ya nyumba, imara yamefungwa, waliomo ndani wahofu, hasira ya mizimu “.Aidha, katika ubeti wa mwisho wa shairi hilo, anaufananisha ushairi wa kimapokeo na kibanda kikuukuu ambacho kinakaribia kuanguka. Hii ina maana kuwa, anauona ushairi huo kuwa umefikia mwisho



na aina mpya ya ushairi, ushairi wa kisasa, unaonekana kutawala. Tazama anasema katika ubeti huu:

“Ni kibanda kikuukuu,  
kuanguka kimekaribia mhimili wake mmoja,  
umeanza kukatika nao mchwa walialia,  
paa si paa tena karibu na huu mhimili,  
katikati ya kibanda kuna kigoda kikubwa,  
ngozi ya chui pambole mbele yake pana moto,  
vijinga vyake mifupa” .

Mbali na kujibizana kupitia mashairi kwenye diwani zao, walijibizana pia kupitia maandiko mengine yasiyokuwa ya kishairi. Majibizano ya aina hii yalioneka pia katika tangulizi za vitabu vyao vya mashairi. Kwa mfano, Abedi (1954) katika dibaji yake anawashambulia washairi wa kisasa na kuwaeleza kuwa hawajui kutunga mashairi na wanashusha thamani ya ushairi wa Kiswahili. Abedi anadai kuwa kuenea kwa vitabu (elimu) na magazeti ndicho chanzo cha kuingia kwa fani hiyo mpya, mashairi ya kisasa, “isiyofaa.” Hebu turejee katika maneno yake anaposema:

Siku hizi kuenea kwa vitabu na magazeti kumewafanya watu wengi watake kutunga mashairi. Mengi mno katika mashairi yanayotungwa, yametungwa bila ujuzi wa kutosha, nayo yaelekea kupunguza thamani ya mashairi ya Kiswahili mbele ya mashairi ya lugha nyinginezo...

Chiraghdin (1980:1) naye anatoa maelezo yanayofanana na Abedi (1954). Yeye anasema kuwa washairi wa kisasa wanauona ushairi kuwa ni mgumu na hivyo hawawezi kutunga

mashairi. Anaendelea kusema kuwa, kwa kuwa hawawezi kutunga mashairi, wanatunga vitu vingine na kudai ni aina mpya ya ushairi. Kwa maelezo haya Chiraghdin anaonekana wazi hakubaliani na wanausasa na anauona kuwa ushairi wao si ushairi wa Kiswahili bali wa Kizungu, hasa wa Kiingereza. Hivyo, Chiraghdin kama ilivyokuwa kwa Abedi (1954) anaonekana kuulaumu ujio wa wakoloni wa Kiingereza pamoja na elimu kuwa ndiyo chanzo cha “kuharibiwa” kwa ushairi wa Kiswahili. Tazama kwa maneno yake anaposema:

Hii leo ushairi umekuwa ni taaluma iliyoenezwa tangu mashule hata vyuo vikuu. Lakini mpaka Leo wanafunzi husikiwa wakilalamika kuwa somo hili ni gumu kwao. Tuseme labda hata hao waliofunzwa Kiswahili wakakishikilia na kuendelea nacho mpaka daraja za utaalumu wa lugha hii na adabu yake, wameuona ushairi wa Kiswahili kuwa ni mgumu mno hata wakaona ni heri waukimbie na wakajizibezibe katika kwapa za kudai kuwa wanauendeleza ushairi huu katika mkondo mpya. Maana kuvyaza kwao si zaidi ya kufuata vipengee vya Kizungu vya kutunga mashairi kwa njia za nathari, na hali humohumo katika fasihi za Kizungu na hata Kiingereza. Wakati mgogoro ulipoonekana kufifia, kulizuka mitindo na mikondo mipya ya kutunga mashairi katika diwani ya *Tunu* ya *Ushairi*. Hatua hii ilizua changamoto mpya kuhusu ufasiri wa dhana ya ushairi na istilahi zinazotumika katika taaluma hii.

## **2.10 Muhtasari**

Sura hii imeshughulikia hatua mbalimbali za maendeleo ya utunzi wa ushairi katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Uchunguzi umebainisha kwamba, kila kipindi maalum cha kihistoria kimeuathiri ushairi wa Kiswahili kifani na kimaudhui. Hatua hii inadhihirisha kwamba juhudi za kutunga hazina kikomo. Kadri siku zinaposonga mbele, ndivyo mikondo na mitindo mipya ya utunzi inavyochipuka na kusababisha changamoto kuhusu ufasiri na maana ya ushairi wa Kiswahili.

Sura inayofuata imechunguza changamoto zinazotokana na mpangilio mpya wa mistari, maneno na upya wa vibwagizo.

## SURA YA TATU

### 3.0 MPANGILIO WA MANENO, MISTARI NA UPYA WA VIBWAGIZO

#### 3.1 Utangulizi

Sura hii iliangalia namna mpangilio wa mistari, maneno na upya wa vibwagizo umejitokeza katika *Tunu ya Ushairi*. Pia, sura hii ilionyesha changamoto zinazotokana na mikondo na mitindo mipya iliyozingatiwa. Aidha, mazingira yaliyochipuzwa aina hii ya utunzi yalishughulikiwa. Mhimili wa nadharia iliyoongoza uhakiki katika sura hii ni pamoja na kauli kwamba muundo wa kazi za kubuni ndio hutumiwa na msanii kutoa ujumbe wake kwa kuangalia jinsi alivyounganisha mawazo yake. Kama vile, alivyounganisha tukio moja na lingine, mistari mmoja na mwingine, ubeti na ubeti. Aidha, muundo wa kazi hutokana na umbo na mpangilio wa kazi ya fasihi. Hili linajibainisha katika kuangalia idadi ya mishororo katika kila ubeti ili kuipa kazi hiyo muundo fulani wa mashairi mbalimbali ya Kiswahili.

#### 3.2 Mpangilio wa Maneno

Kipengele cha mpangilio wa maneno katika diwani ya *Tunu ya ushairi* kinadhihirisha mikondo mingi ya pindu kama inavyojitokeza katika mashairi ya *Risala za Amani* na *Lauzi mwanangu*. Pindu ni shairi lililotungwa kisanaa ili kwamba kipande cha mwisho wa mshororo au neno la mwisho la ubeti linatumiwa kuanzisha mshororo unaofuata au ubeti unaofuata. Haya ni kwa mujibu wa kaida za utunzi wa mashairi yaliyozoeleka. Katika diwani ya *Malenga wa Ziwa Kuu*, vile inavyowakilisha bahari ya pindu ni ile njia ambayo imezoeleka. Mfano wa shairi la pindu katika diwani hii ni;

**MCHEZA KWAO HUTUZWA UK.(154)**

*Kulia aliye mwelewa, aghalabu hupongezwa*

*Hupongezwa na kupawa, tunu bora ya kutuzwa*

*Kutuzwa na kuambiwa , wanasi wamependezwa*

*Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiriwa*

*Au la hushangiriwa, bila hata kupuuzwa*

*Wapuuzwa atakuwa, simanzi tele kajazwa*

*Kajazwa pia ukiwa, badala ya kuhimizwa*

*Mcheza kwao hutuzwa, au la hushangiliwa.....*

Kutokana na mfano huu, kipande cha mwisho cha mshororo kinatumiwa kuanzisha mshororo unaofuata au ubeti unaofuata. Diwani ya *Tunu ya ushairi* inabainisha upya mwingi katika kuwasilisha dhana ya shairi la pindu. Kwa mfano, katika shairi la *Risala za Amani*, kuna mikondo ifuatayo ya pindu. Kwanza , neno linalomalizia kipande cha kwanza cha mshororo, linachukua umbo tofauti na kuanza kipande cha pili cha mshororo huo. Aidha, maumbo na maana huwa tofauti. katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza, neno *Risala* linabadilika na kuwa *sala*, na katika mshoro wa pili, neno *kabila* linabadilika na kuwa *bila*. Mshororo wa tatu neno *ukabila* linabadilika na kuwa kabila na katika mshororo wa nne, neno *mila* linabadilika na kuwa *ila*.

Mifano;

### **Risala za Amani**

*Tungo peleka risala, sala kwa Mwenyezi Mungu*

*Na watu kila kabila, bila kujali mnengu*

*Waambie ukabila, kabila lao na langu*

*Si neno pamwe na mila, ila zote walimwengu*

Neno risala lina maana ya taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani inayoeleza haja inayotakiwa. Sala kwa upande mwingine ina maana ya maombi kwa Mwenyezi Mungu.

Kabila ina maana ya kikundi cha watu katika taifa wanaohusiana kwa lugha, mila, desturi na utamaduni. Bila ina maana ya kutokuwa nayo, pasipo au sufuri.

Ukabila maana yake ni hali ya kupendelea kabila moja na watu wao huku wakiona wao ni bora kuliko kabila zingine. Ilhali kabila ina maana ya kikundi cha watu katika taifa wanaohusiana kwa lugha, mila, desturi na utamaduni. Neno mila lina maana ya mambo yanayofanywa na sehemu kubwa ya jamii fulani yanayolingana na asili na utaratibu wa nyendo za jamii hiyo. Maneno haya kuanzishwa katika kipande cha pili cha mshororo na kubadili maana yake huzua changamoto kwa wahakiki wa mashairi kuhusu dhana ya pindu kama ilivyozoeleka.

**Mfano wa pili;****Lauzi, Mwanangu***Ewe mwanangu Lauzi, Lauzi binti yangu**Zidarizi beti hizi, hizi wasia wangu**Ukuapo umaizi, umaizi ulimwengu**Kwamba hauna mjuzi, mjuzi wa ulimwengu**Hajawapo pande hizi, hizi toka babu zangu**Tangu kuwepo Wangozi, Wangozi hata Wazungu**Kila aliye ajizi, ajizi yake ni pingu**Kisha hulewa ulezi, ulezi wa ulimwengu**Usiokuwa na mbawazi, mbawazi ila machungu**Yasikufike mwanangu, mwanangu nakuusia*

Shairi hili halifuati ile hali iliyozoeleka kuhusu dhana ya pindu. Neno linalomalizia kipande kimoja linaanza katika kipande cha pili na si mshororo. Hali hii huweza kuzua changamoto katika kuelezea maana ya pindu. Bahari ya kikwamba nayo imechukua mikondo mbalimbali. Miongoni mwa mashairi yanayodhihirisha mikondo ya bahari hii ni pamoja na *Pendo la Pesa na Rai* na *Mawaidha*.

Kulingana na maelezo ya dhana iliyozoeleka ya kikwamba, inafafanuliwa kama shairi ambalo kila ubeti au mshororo huanza kwa neno moja linalorudiwa, na neo hilo huwa na

maana sawa katika shairi zima. Mfano unaodhihirisha dhana hii ni wa shairi kutoka *jopo la Kiswahili la Thika* katika mfano ufuatao.

**Panda (Ukurasa wa 44)**

*Panda, panda la mnazi, l'anzalo kupapatuwa*

*Panda juu ya malezi, moyo wako wishe ngowa*

*Panda mti wa mapenzi, uwepushie na juwa*

*Panda ni wako uluwa.Panda darajari, Panda!*

*Panda juu ya farasi, kwa haiba na sitawa*

*Panda kiwango mkwasi, uukimbie ukiwa*

*Panda, situpe viasi, wendako ukikujuwa*

*Panda, ni wako uluwa.Panda darajani, Panda!.....*

Neno panda, licha ya kuwa na maana mbalimbali, katika shairi hili lina maana sawa na limetumika kuanzisha kila mshororo katika kila ubeti.

Katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*, kuna upya katika kuwasilisha bahari ya kikwamba.

Mfano 1;

**Kanwa Langu Pima Neno**

*Kanwa nena, neno, lenye kupendeza*

*Baya kana,neno, ovu lachikiza*

*La maana,neno,jema linafunza*

*Kanwa pima neno.*



*Kanwa pimwa, neno, kwanza lichunguza*

*Lenye chama, neno, kuliiza*

*Neno jema, neno, kwa anosikiza*

*Kanwa pima neno*

Kutokana na mfano huu, neno ambalo limerudiwa katika shairi hili ni *nen*o lakini halifuati ule mkondo ambao umezoeleka katika kufasili dhana ya kikwamba. Halitumiki katika kuanzisha mshororo katika ubeti. Badala ya kuanza mshororo, linapatikakana katikati mwa mshororo.

Mfano 2;

### **Rai na Mawaidha**

*Umbea kasema babu, umbea magaragaza*

*Umbea ukhutubu, umbea takufukuza*

*Umbea si matulubu, umbea utateleza*

*Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu*

*Umbea unaharibu, umbea si kupendeza*

*Umbea si mahisabu, umbea katu kujaza*

*Umbea ni majisibu, umbea unapunguza*

*Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu*

*Umbea ujishurubu, umbea kuukataza*

*Umbea tujitanibu, umbea mbali kusoza*

*Umbea si njema gubu, umbea si mwangaza*

*Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.*

Katika shairi hili, kuna upya pale ambapo neno *Umbea* limetumika katika kipande kimoja cha mshororo na kuanza tena katika kipande cha pili. Ule mtindo uliozoeleka unakiushwa kwa vile neno hilo limetumika mara mbili katika mshororo mmoja na kuweza kuibua changamoto katika kufasili dhana ya kikwamba.

### **3.3 Mpangilio wa Mistari**

Kwa mujibu wa kigezo cha mpangilio wa mistari katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*, yapo mashairi yenye mstari mmoja katika kila ubeti hadi ya mistari kumi katika kila ubeti. Kuna hata shairi lenye mistari kumi na minne katika kila ubeti. Mashairi ambayo yamezoeleka sana ni yale ya tarbia, takhmisa na hata lile la tathlitha. Lakini diwani ya *Tunuya U shairi* ina upya mwingi pale ambapo mashairi yanajitokeza ya mstari mmoja hadi kumi na minne.

Mfano 1;

**TUNGATAMANI (173)**

*Tungatamani dunia, yenye uingi wa raha, haiji bila taabu*

*Tungatamani ushindi, tushinde hata karaha, hauji bila kushindwa*

*Tungatamani takaso, litutie na furaha, ila nyoyo ni dhaifu*

*Tungatamani kudumu, tusipungukiwe siha, ila maisha husita*

*Tungatami ushwari, usotumbua usaha, ila wimbi halikosi*

*Tungatamani kwongoza, uongozi wa staha, ila nahodha adimu.....*

Kile ambacho kinaonekana kuwa ni mshororo mmoja ni ubeti uliokamilika kwa sababu unabeba ujumbe kamili. Shairi la mstari mmoja ni nadra sana kupatikana katika ule mtindo uliozoeleka. Diwani ya *Tunu ya Ushairi* inapita mipaka hadi kuwa na shairi la mistari kumi na minne.

Mfano 2;

**Tusitete (115)**

*Washairi tupendane, tusitete*

*Tama na tutiane, tusikate*

*Kutunga tuhimizane, tusiwape*

*Daima tushikamane, kama kete*

*Kwenda mbele tukazane, tujikite*

*Hadhi na tija nyingine, tukapate*

*Isiwe tufarakane, bali sote*

*Heshima tuekeane, wenye kite*

*Wabakie na mavune, tusitete*

*Wala tusichukiane, tusifute*

*Nakukashifu wengine, sisi sote*

*Waandishi tuungane, kule kote*

*Na huku hata kwingine, siku zote*

*Kwa mazuri tuigane.....*

Shairi hili limefuata arudhi. Lina vina vya ndani, na vya nje. Tukiangalia ubeti wa kwanza, limefuata mkondo wa kikai, pale ambapo kipande cha kwanza kina mizani nane na nne. Pia kibwagizo chake kimefupishwa kuchukua mkondo wa msuko. kisha, katika kuangalia ubeti wa pili, kipande cha kwanza kimechukua umbo la mizani nne kwa nane. Kwa hivyo linachukua mikondo mbalimbali, kumaanisha kuwa katika ile hali iliyozeleka inafaa kuitwa sakarani.

Mashairi haya yanazua changamoto kwa vile hayajazoeleka katika kuyafasili. Hivyo, mikindo inayofuatwa haijazoeleka katika ufasili na uchambuzi wa mashairi uliozoeleka.

### **3.4 Upya wa Vibwagizo**

Kibwagizo ni mshororo wa mwisho katika ubeti ambao unajirudiarudia kulingana na maelezo yaliyozoeleka. Maelezo haya yanadhihirishwa kutokana na mifano kutoka diwani ya Jopo la Kiswahili la Thika.

Mfano 1;

#### **BURIANI**

*Ndugu aliye muhibu, kaaga nenda mjini*

*Nikasake ya wajibu, na kutia jicho shani*

*Takayefika mjibu, sendi kawia mjini*

*Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa*

*Kituoni alingoja, usafiri ni wajibu*

*Mara gari hilo laja, kaingia bila tabu*

*Kumbe vile ni mauja, yangoja wetu muhibu*

*Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa*

*Dereva kawa kituko, kaendesha kwa mikogo*

*Sukani huku na huko, kauvuta kama gogo*

*Kichwa chake sawa kuko, kajaza pombe ni zigo*

*Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa.....*

Kibwagizo katika mfano huu ni; Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa.

Mfano 2;

Katika diwani ya *jinamizi* (1979).

**NGAZI UK. (22)**

*Ngazi hii ya ajabu, mwanangu nakuundia*

*Navipanga kwa hisabu, vidato vya kupandia*

*Cha awali ni adabu, wenzako kuwafanyia*

*Mti wake maalum, radhi ya baba na mama*

*Sikiza ewe ghulamu, leo nakupa wasia*

*Mambo yenda kwa nidhamu, haitoshi kuwania*

*Na cha pili ni elimu, japo ngumbaro pitia*

*Mti wake maluum, radhi ya baba na mama*

*Beti hii ni tukufu, na fasaha kutimia*

*Iwe kwako uraufu, upate kuzingatia*

*Cha tatu uadilifu, uwatendee raia*

*Mti wake maalum, radhi ya baba na mama.....*

Kibwagizo katika mfano huu ni; Mti wake maalum, radhi ya baba na mama.

*Tunu ya Ushairi* imetumia mikondo mipya katika kuiwasilisha dhana ya kibwagizo. Upya huu umejidhihirisha katika mashairi *Nilikupa Ukatupa, Siku Zimesonga na Vipande Viwili*

Mfano 1;

**Nilikupa Ukatupa UK. 77**

*Nilikupa, kila changu, ukatupa*

*Nilikupa, dhati yangu, ukatupa*

*Nilikupa, moyo wangu, ukatupa*

*Nilikupa, siri yangu, ukatupa*

*Nilikupa, kila change, ukatupa*

*Nilikupa, roho yangu, ukatupa*

*Nilikupa, wema wangu, ukatupa*

*Nilikupa, mwili wangu, ukatupa*

*Nilikupa, ngeu yangu, ukatupa*

*Nilikupa, kila changu, ukatupa*

*Nilikupa, chembe yangu, ukatupa*

*Nilikupa, utu wangu, ukatupa*

*Nilikupa, utu wangu, ukatupa*

*Nilikupa, jina langu, ukatupa.....*

Kutokana na mfano huu, kibwagizo kimejitokeza kwa njia mbili. Katika kipande cha kwanza cha neno *Nilikupa* na kipande cha pili cha kila mshororo katika neno *Ukatupa* na kuwa na ujumbe na msisitizo tofauti. Pia, kibwagizo kimejitokeza katika kila mshororo wa kwanza wa ubeti pale ambapo mshairi ametumia mshororo; *Nilikupa, kila changu, ukatupa* katika kila ubeti mwanzoni na kuweza kukifanya kuwa kibwagizo. Hali hii ni tofauti katika kufasili dhana ya kibwagizo na ile ambayo imezoeleka na kupelekea kuzua changamoto ya kufasili dhana hiyo ya kibwagizo.

Mfano 2;

**Siku Zimesonga uk. 123**

*Ulikuwa utarudi!*

*Sikudhani ungerudi, mahaba yalivyokonga*

*Kusubiri ingebidi, ela siku zimesonga*

*Nilibaki sina budi, ila mlango kufunga*

*Ulikuwa utarudi!*

*Nilidhani kafaidi, huko ulikwenda tanga*

*Japo endaye hurudi, ela siku zimesonga*

*Mpendwao muna kedi, hamuishi kujiringa*

*Ulikuwa utarudi!*

*Moyo ulitaradi, kasha ukatia nanga*

*Ninasikia hodi, ela siku zimesonga*

*Wanamba wangu fuadi, huba limesha jitenga*



*Ulikuwa utarudi!*

*Kuwepo kwako baidi, majuto yalinisonga*

*Na ingawa umerudi, ela siku zimesonga*

*Pendo sipi mkaidi, japo nikatwe mapanga*

Vibwagizo ni viwili katika shairi hili. *Ulikuwa utarudi* na *ela siku zimesonga*. kimejitokeza mwanzoni na pia katikati mwa shairi hilo na hasa kinajitokeza katika kipande cha pili cha mshororo wa tatu wa ubeti. Watunzi hawa wanachukua mikondo mipya ikilinganishwa na ile ambayo imezoeleka kuhusiana na dhana ya kibwagizo na kuzua changamoto kwa ile dhana iliyozoeleka ya kibwagizo. Na jinsi hii, kunahitajika maelezo mapya kuhusiana na hali hii ili iendane na hali ya sasa ya dhana hii kwa sababu maelezo ya zamani kuhusu dhana hii haifasili vyema dhana hii katika hali ya sasa.

Mfano 3;

**Vipande Viwili UK. 160**

*Tangu liliporaruka, huba vipande viwili*

*Ni mengi yamenifika, mradi kunithakili*

*Nusura niwe mahoka, kwa vurugu la akili*

*Nimebakia hamali, moyo hukunisali*

*Tangu liliporaruka, huba vipande viwili*

*Kila saa na dakika, asubuhi na laili*

*Roho yanipapatika, sikai wala silali*

*Nimebakia hamali, moyo hukunisaili*

*Tangu liliporaruka, huba vipande viwili*  
*Mno nimehangaika, kamwe sijatua tuli*  
*Mwili umedhoofika, na ubongo na akili*  
*Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.....*

Shairi hili vilevile lina vibwagizo viwili. Moja kujitokeza mwanzoni mwa ubeti; *Tangu liliporaruka, huba vipande viwili* na mwisho wa ubeti; *Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.*

### **3.5 Muhtasari**

Kuna mikondo mipya ya kutunga mashairi tofauti na maumbo yaliyozoeleka. Hali hii inajitokeza katika vipengele vya maneno, mistari na vibwagizo. Hali hii inazua changamoto katika uhakiki wa mashairi katika hali yake ya sasa. Kwa hivyo, kuna haja ya dhana zilizozoeleka kuchunguzwa upya ili kuafiki hali ya sasa ya utunzi wa mashairi.

## SURA YA NNE

### 4.0 USHAIRI HURU, USHAIRI PICHA NA USHAIRI ARUDHI

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia upya katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake na kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi. Aidha, inabainisha mitindo ya kutunga mashairi ya awali na namna inavyoweza kuendelezwa kwa namna nyingine ya utunzi. Sura hii imeongozwa na mhimili wa nadharia usemao ya kwamba maudhui na dhamira hushughulikia falsafa ya mtunzi kuhusu jamii anayozungumzia. Pia, muundo wa kazi hutokana na umbo na mpangilio wa kazi husika ya kifasihi.

#### 4.2 Upya katika Namna ya Kuwasilisha Ushairi Arudhi katika Bahari Zake

Ngonjera ni mojawapo ya mashairi arudhi ambayo katika bahari zake, yamedhihirisha upya katika diwani ya *Tunu*. Kulingana na maelezo yaliyozoeleka, ngojera ni shairi lenye wahusika wawili wanaojibizana. Mfano kutoka diwani ya *Jopo la Kiswahili la Thika* kushadidia maelezo ya ngojera ni shairi la;

#### **Tamadunizo Siase (Ukurusa 51)**

*Dada Umbu hayo ni kusudi, au ndiyo miujiza?*

*Nakuona meshitadi, kulia jambo waigiza,*

*Ndipo kawa sina budi, leo kweli kukujuza,*

*Usije kajipoteza, tamadunizo kuasa*

*Dada kaka hela tabarudi, moto wako kupunguza,  
Naona wataradadi ukuhani kujikweza,  
Ni wako upi muradi, utakao kunijuza?  
Nambie naloigiza, ni utamaduni gani?*

*Kaka Mbona waja kali sasa, name nakuelekeza?  
Tuongee kisiasa, hai mana kuchagiza  
Kuigiza ndicho kiza, khususa kizungumza,  
Wajifanya Mngereza, ni utamaduni gani?*

*Dada Kaka wafanya makosa, kisema nimeigiza  
Sababu metowa pesa, lugha hii kujifunza  
Mejifunza kwa mikasa, kichapwa nikijikaza,  
Hela nalouigiza, ni utamaduni gani?.....*

Mfano wa pili ni shairi kutoka mashairi ya (Masinde, 2007), Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili na Vyu;

### **Uhaba wa Kazi**

*Kaka Kusoma nilikosoma, kambiwa sipati kazi,  
Yapata mwaka mzima, nategemea shangazi,  
Wasiojua husema, 'sababu sina ujuzi,  
Huno uhaba wa kazi, mesababishwa ni wake.*

*Dada Mbona watuingilia, kaka acha ubaguzi,  
Likukeralo twambia, tulijuwe waziwazi,  
Au analochukia, ni wake kufanya kazi?  
Mambo ya kisiku hizi, watu ni bega kwa bega.*

*Kaka Siwaingilie kwa nini, nanyi mwatupoka kazi?  
Kwani tokea zamani hazikuwa shida hizi,  
Mtu kitoka shuleni kibarua si tatizi,  
Leo hatupati kazi, kisa nyingi wanawake.....*

*Tunu ya ushairi ina upya mwingi katika kuwasilisha bahari ya ngojera. Mifano ya mashairi yanayodhihirisha hali hiyo ni pamoja na “Bwana na mke na Baraka na Ali”.*

### **Bwana na Mke**

*Bwana: U hali gani azizi?*

*Mke: Hali yangu njema*

*Bwana*

*Bwana: Khabari za matembezi?*

*Mke: Kwa kweli salama sana*

*Bwana: Wa'hali gani wazazi?*

*Mke: Wote wazima kibwana*

*Wote: Twashukuru kukutan, sisi wapenzi wawili*

*Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali*

*Bwana: Ilikuwaje safari?*

*Mke: Bwana nashindwa kunena*

*Bwana: Ilikuwa ya Khatari?*

*Mke: Hapana Bwana hapana*

*Bwana: Ilikwenda vizuri?*

*Mke: Kama unavyoniona*

*Wote: Twashukuru kukutana, sisi wapenzi wawili*

*Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali.....*

Umbo hili la ngonjera lina upya katika uwasilishaji wake. Ngojera iliyozoeleka ina mpangilio tofauti na huu wa diwani ya *Tunu*. Wanakutana wote kwa kiitikio tofauti na ngojera iliyozoeleka.

### ***Baraka na Ali***

***B: Hodi hodi bwana Ali, hodi ndani samahani!***

***A: Karibia tafadhali, karibu ingia ndani.***

***B: Nakushukuru kikweli, kwa karibu ya hisani.***

***A: Umetoka huko mbali, azma yako ni nini?***

***B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.***

***A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.***

***B: Tunamshukuru sana, kwa mapenzi ya moyoni.***

***A: Tabia ya kuonana, si leo tangu zamani.***

***B: Ni kweli unayone, hayapati ukinzani.***

***A: Ama watu kupendana, humpendeza manani.***

*B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.*

*A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.*

*B: Lakini Bwana Bakari, habari gani shambani?*

*A: Kuna mavuno mazuri, kwa chakula cha mwakani.*

*B: Na sisi kwetu tayari, mavuno yamo gharani.*

*A: Neema jambo la kheri, nchi huwa furahani.*

*B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.*

*A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.*

*B: Haya tuagane, tuagane kwa kherini.*

*A: Na tuombe tuonane, kwa afya njema mwilini.*

*B: Na tuombe tushikane, kama pete kidoleni.*

*A: Kwa mema tuhimizane, ndugu na zetu jirani.*

*B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.*

*A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.*

Shairi hili lina upya kwa vile tunaona mwandishi hatambui wahusika kwa majina yao, bali katika herufi *A* na *B*. Majibizano yanapatikana katika mshororo badala ya kila ubeti kulingana na hali iliyozoeleka. Ubunifu huu unahutajirisha ushairi wa Kiswahili.

#### **4.3 Kujumuishwa pamoja Ushairi Huru, Ushairi Picha na Ushairi Arudhi**

Diwani ya *Tunu* ina mkusanyiko wa mashairi ambayo yamefungua ukurasa mpya katika utunzi wa mashairi.

Katika diwani ya *Tunu* ya *Ushairi*, upya pia unajitokeza pale ambapo kuna kujumuishwa pamoja uhairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi. Hali hii inaleta uwiano kati ya wanamapokeo na wanamapinduzi kuwa ubunifu umepanuka na hainabudi kukubali maendeleo hayo ili kuutajirisha ushairi wa Kiswahili. Mashairi arudhi ni yale yanayozingatia kanuni za utunzi wa mashairi kama vile idadi ya mishororo, vina, mizani, beti, bahari na kibwagizo. Mifano ya mashairi arudhi kutoka diwani ya *Tunu* ni pamoja na; *Wasia, Hili na lile naTunu*.

Mashairi huru ni mashairi yasiyozingatia kanuni za utunzi wa mashairi. Mashairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa mashairi. Anaweza kufanya makosa kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani.



Mifano ya mashairi huru ni pamoja na; *Monyara, Sina Hakika, na Vifusi vya Damu*

***Monyara uk 101***

*Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara*

*Tuliochelea kukaribia kingo zake*

*Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia*

*Kwa kunyenyekea wingi wa yake maji*

*Yaliyojiendea utadhani yamesimama*

*Ni katika mto huu*

*Ambapo samaki wakubwa tulivua*

*Maguo kutatakasa japo kwa kuunyemelea*

*Na walevi stadi wakachelea kuuvuka*

*Ulipofura na kupita kwa kiburi*

*Kwa kushiba maji yake*

*Yaliyofanya mawimbi madogo.....*

Mfano wa pili wa shairi huru ni;

***Sina Hakika! Uk wa 109***

*Mimi tena sina tofauti*

*Na chumvi iliyoguzwa na maji:*

*Ukali umo kasoro udhahiri*

*Mlima wakodoa macho mbele yangu*

*Kiini cha ngoma kinazidisha mlio*

*Natulia na kujisaili.*

*Natambua u pale pale*

*Unanitizama*

*Unanihimiza kimyakimya*

*Nahisi unanidara*

*Lakini*

*Sina hakika!*

*Upeo wake umeongezeka maradufu*

*Katika kiini cha damu na fikra zangu*

*Ninapiga hatua*

*Kila mguu wauhimiza mwenziwe kuanza*

*Naona kama yote inasonga*

*Wakati huo huo unasita*

*Kama kuuomba moyo idhini!*

*Moyo unacheka sawia na mlima*

*Nasikia maneno Fulani*

*Sina hakika ni sauti au fikra:*

*Ni kanuni hii*

*Mimi bado nipo*

*Siku zote ulinikanyaga*

*Na uso kuniparua*

*Wala sikulalamika*

*Mwenyewe utakapochoka usihofu*

*Tumboni nitakusetiri*

*Lakini kwa sasa tamba*

*Japo kwa kuogopa*

*Hii awamu ya lala salama!*

Mtunzi wa shairi hili ametumia uhuru wake kuongeza idadi ya mishororo kila anapotoka ubeti mmoja kuelekea ubeti mwingine. Hajafungwa na sheria yoyote katika utunzi wake. Mashairi picha nayo ni mashairi ambayo muundo wake si wa kawaida, ambapo mshairi anaandika shairi lake na kulifanya lito e picha fulani kulingana na dhana anayoishughulikia mshairi. Mashairi ya aina hii yanaiongezea diwani hii upekee. Mifano ya mashairi picha ni pamoja na; *Ni makini, Siondoki, Ndumilakuwili, Vidato vya Maisha* na *Maisha Vidato*. Mashairi haya yanajitokeza katika diwani ya *Tunu* yakiwa na ujumbe fulani katika picha hiyo.

**Ndumilakuwili uk. 146***Mbona waleta utata**Wa mambo kuyavuruga?**Mbona huishi papara**Na nyingi**a k**l u**i w**m i**u l**d i**n ?**Keti, tulia, makinika, tafakari**Sote tuketi chini hapa**Chini ya hili letu jingo**Pamoja tufanye shirika**Shirika la shikamano**Kabla giza kutanda*

Shairi la *Ndumilakuwili* lina picha ya nyumba. Kwamba, kama kuna ushirikiano na kuacha vurugu, nyumba hiyo inakamilika na kusimama imara.

Mfano wa pili wa shairi picha kutoka diwani ya *Tunu ya Ushairi* ni “siondoki”

**Siondoki uk.87**

*Eti*

*Niondoke!*

*Mimi niondoke hapa*

*Niondoke hapa kwangu!*

*Nimesaki; licha ya risasi*

*Vitisho na mauaji, siondoki.*

*Mimi*

*Siondoki*

*Siondoki siondoki*

*Niondoke hapa kwangu!*

*Kwa mateke hata na mikuki*

*Marungu na bunduki, siondoki*

*Hapa*

*Siondoki*

*Mimi nipahame!*

*Niondoke hapa kwangu!*

*Fujo na ghasia zikizuka*

*Na kani ya waporaji, siondoki.....*

Mfano wa shairi picha kutoka diwani ya *Tunu* ni;

**Vidato vya Maisha uk.59**

*Vidato*

*Vya*

*Maisha*

*Mithili*

*ya*

*sarafu;*

*kipo*

*kichwa*

*nao*

*wa*

*pili*

*upande.*

*Kuna*

*Kupanda*

*na*

*kushuka,*

*kupenda*

*na*

*kuchukia*

*kufaulu*

*na*

*kushindwa.....*

Shairi hili lina picha ya ngazi. Limechukua umbo hili kuwasilisha hali ya maisha katika pandashuka zake. Maisha yana changamoto zake. Kuna kufaulu na kufeli. Mshairi anatuelezea kuwa , vyovyote vile, hiyo ni hali ya maisha.

#### **4.4 Muhtasari**

Sura hii imeshughulikia hali ya upya katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake na kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi. Tumbainisha kuwa watunzi wamevuka mipaka ya mgogoro wa ushairi hadi kujumuisha bahari zote za mashairi pamoja. Hali hii huondoa mipaka iliyokuwepo awali iliyotenganisha ushairi arudhi na ushairi huru ili kuonyesha ya kwamba, mitindo ya kutunga mashairi ya awali inaweza kuendelezwa kwa namna nyingine katika harakati za kujirekebisha na kujiunda upya na kuendana na mahitaji ya kiwakati.

## SURA YA TANO

### 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii muhtasari wa utafiti umetolewa. Aidha, lengo kuu la utafiti limeelezwa pamoja na upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura. Vilevile, matokeo ya utafiti yameelezwa kwa undani kwa kuonyesha jinsi utafiti ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo yake. Pia, mchango wa utafiti umeelezwa na hatimaye mapendekezo ya tafiti za baadaye yametolewa.

#### 5.2 Muhtasari

Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu. Kwanza, kubainisha mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*, kubainisha mazingira yanayochipuzwa mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi na changamoto zinazotokana na mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi.

Utafiti huu ulitokana na sababu kuwa kuna mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi katika *Tunu ya Ushairi*, jambo ambalo limezua changamoto kuhusu ufasili na uchanganuzi wa mashairi ya Kiswahili. *Tunu ya ushairi* iliteuliwa kimakusudi kwa ambavyo ndiyo diwani ya hivi karibuni na iliyo na mitindo na mikondo mipya ya utunzi. Kwa jinsi hii, imezua changamoto katika uchambuzi wa mashairi ya Kiswahili. Jumla ya



mashairi kumi na nane yaliyoteuliwa kila kipengele kuchukua mashairi yanayojitosheleza kimaelezo.

Mazingira yamechangia pakubwa katika kuibua mbinu mpya za utunzi na kupelekea kuzua changamoto katika kufasili dhana mbalimbali za ushairi kama vile kibwagizo, mpangilio wa mistari na mpangilio wa maneno. Mikondo na mitindo mipya ya utunzi inatufanya tukubali kuwa dhana mbalimbali za ushairi zinafaa kuchunguzwa upya, kubadilishwa na kupanuliwa kulingana na hali ya sasa ya viwango vya ubunifu katika utunzi wa ushairi.

Katika kufikia malengo yetu, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kimtindo inayosisitiza kuwa ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani, lazima vipengee vinavyofanya kazi hiyo ivutie vizingatiwe. Navyo ni kama vile matumizi ya taswira, uteuzi wa maneno, urari wa vina na mahadhi ya mashairi.

Utafiti ulichukua muundo wa kimaelezo na utafiti ulifanyika maktabani kupitia usomaji wa kina na udondoaji wa mifano mwafaka. Sampuli ilituuliwa kimakusudi ambapo mashairi kumi na nane yaliteuliwa. Ukusanyaji data ulifanywa kwa njia ya usomaji wa kina na udondoaji wa mifano mahususi. Uchanganuzi wa data uliongozwa na malengo, maswali ya utafiti, mihimili ya nadharia na pengo la kushughulikiwa. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji wa mifano.

Tasnifu iligawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi ilishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti, na udurusu wa maandishi juu ya mada. Sura hii pia imeangazia mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganguzi na uwasilishaji wa matokeo.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia historia, maendeleo na mabadiliko ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili kwa lengo la kuonyesha maendeleo na mabadiliko katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

Sura ya tatu ilishughulikia namna mpangilio wa mistari, maneno na upya wa vibwagizo umejitokeza katika *Tunu ya Ushairi*. Pia, sura hii imeonyesha changamoto zinazotokana na mikondo na mitindo mipya iliyojitokeza katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Aidha, mazingira yaliyochipuzwa aina hii ya utunzi yalishughulikiwa.

Katika sura ya nne, utafiti ulishughulikia vile mashairi ya aina zote yalivyojumuishwa pamoja katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Mikondo mipya ya kushughulikia mashairi arudhi katika bahari zake mbalimbali pia ilishughulikiwa.

### 5.3 Matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti yalishughulikiwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kuhusu lengo la kwanza ambalo ni kubainisha mikondo na mitindo mipya ya utunzi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi*, utafiti ulipata kuwa kuna mikondo mipya ya kutunga mashairi, tofauti na maumbo yaliyozoeleka. Hali hii inajitokeza katika vipengele vya maneno, mistari na vibwagizo.

Kutokana na kipengele cha mpangilio wa maneno, mikondo mipya ilijitokeza katika diwani ya *Tunu ya ushairi* kwa kuzingatia dhana ya pindu, kama inavyodhihirishwa katika mashairi ya *Risala za Amani* na *Lauzi mwanangu*. Katika mashairi hayo, neno linalomalizia kipande cha kwanza cha mshororo, linachukua umbo tofauti na kuanza kipande cha pili cha mshororo huo. Aidha, maumbo na maana huwa tofauti tukizingatia ile hali ambayo imezoeleka kuhusiana na dhana ya pindu.

Mikondo mipya pia ilijitokeza katika istilahi ya kikwamba. Miongoni mwa mashairi yaliyodhihirisha mikondo ya bahari hii ni pamoja na *Pendo la Pesa* na *Rai na mawaidha*. Upya ulijitokeza katika kuangalia maumbo ya mashairi haya. Hususa, neno ambalo limerudiwa katika shairi la *Pendo la Pesa* halifuati ule mkondo ambao umezoeleka katika kufasili dhana ya kikwamba. Halitumiki katika kuanzisha mshororo katika ubeti wa ushairi. Badala ya kuanza katika mstari linapatikakana katikati mwa mshororo.

Katika shairi la *Rai na Mawaidha*, kuna upya pale ambapo neno *Umbea* limetumika katika kipande kimoja cha mshororo na kuanza tena katika kipande cha pili. Ule mtindo uliozoeleka unakiushwa kwa vile neno hilo limetumika mara mbili katika mshororo mmoja.

Kuhusu kipengele cha mpangilio wa maneno, mikondo mipya ilijitokeza ambapo utafiti ulipata kuwa kuna shairi la mstari mmoja hadi shairi la mistari kumi na minne. Mifano inayodhihirisha mikondo hiyo ni shairi la *Tungatamani* na *Tusitete*.

Mikondo mipya pia ilijidhihirisha katika dhana ya kibwagizo. Upya unajitokeza katika mashairi *Nilikupa Ukatupa*, *Siku Zimesonga* na *Vipande Viwili*. Katika shairi la *Nilikupa Ukatupa*, kibwagizo kinajitokeza kwa njia mbili. Katika kipande cha kwanza cha neno *Nilikupa* na kipande cha pili cha kila mshororo katika neno *Ukatupa* na kuwa na ujumbe na msisitizo tofauti. Pia, kibwagizo kinajitokeza katika kila mshororo wa kwanza pale ambapo mshairi ametumia mshororo; *Nilikupa*, *kila changu*, *ukatupa*.

Vibwagizo ni viwili katika shairi la *Siku Zimesonga*. Vibwagizo hivyo ni; *Ulikuwa utarudi* na *ela siku zimesonga*. Vimejitokeza mwanzoni na pia katikati mwa shairi hilo na hasa katika kipande cha pili cha mshororo wa tatu wa ubeti wa shairi hilo. Vilevile, katika shairi la *Vipande Viwili*, shairi hili lina vibwagizo viwili. Moja kujitokeza mwanzoni; *Tangu liliporaruka, huba vipande viwili* na mwisho wa ubeti; *Nimebakia hamali, moyo hukunisaili*.

Katika sura ya nne, mikondo na mitindo mipya ilijitokeza katika namna ya kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake na kujumuishwa pamoja ushairi huru, ushairi picha na ushairi arudhi. *Tunu* ya *ushairi* ina upya mwingi katika kuwasilisha bahari ya ngojera. Mifano ya mashairi yanayodhihirisha hali hiyo ni pamoja na *Bwana* na *Mke* na *Baraka* na *Ali*.

Shairi la *Bwana na Mke* lina upya pale ambapo mtunzi hataji wahusika kwa majina yao, bali katika herufi *A* na *B*. Majibizano yanapatikana katika mshororo badala ya kila ubeti kulingana na hali iliyozeleka.

Shairi la *Baraka na Ali* linadhihirisha mikondo mipya kwa vile lina kiitikio kinachowaunganisha wote wawili. Katika ujumuishwaji wa aina za mashairi, kuna mashairi arudhi kutoka diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Mifano; *Wasia*, *Hili na lile* na *Tunu*.

Mashairi huru yanajidhihirisha katika mifano ifuatayo; *Monyara*, *Sina Hakika*, na *Vifusi vya Damu*. Mifano ya mashairi picha ni pamoja na; *Ni makini*, *Siondoki*, *Ndumilakuwili*, *Vidato vya Maisha* na *Maisha Vidato*. Mashairi haya yanajitokeza katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* yakiwa na ujumbe fulani katika picha hiyo. Aina zote za mashairi zinajumuishwa katika diwani moja kinyume na diwani nyingi zinazosisitiza mashairi arudhi.

Kuhusiana na lengo la pili ambalo ni kubainisha mazingira yaliyochipuza mikondo na mitindo mipya ya utunzi wa mashairi, matokeo yanaonyesha kuwa, katika kipindi cha

miaka ya 1960 kulishuhudiwa mabadiliko ya kifani yaliyotokana na kuibuka kwa ushairi wa kisasa. Mabadiliko haya yanaitwa majaribio katika ushairi. Utafiti ulipata kuwa majaribio yamekuwapo katika tanzu mbalimbali za fasihi. Mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili yalianza tangu mwishoni mwa miaka ya 1960 lakini yakashika kasi sana na kuwa bayana zaidi katika kipindi cha sasa ambapo *Tunu ya Ushairi* imetungwa.

Baada ya uhuru, tukio muhimu lilikuwa kwamba, katika utunzi wa mashairi kulikuwa na mwamko mpya wa kutunga mashairi yasiyofuata arudhi. Na hayo ndio mazingira yaliyochipuzwa aina mpya ya utunzi. Uhuru wa kisiasa ulikuwa na athari kuu katika jamii husika. Mapokeo yote yalichunguzwa upya likiwemo suala la namna ya kutunga mashairi ya Kiswahili. Jambo hili lilizua hali ambapo watunzi wapya kama vile Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi miongoni mwa wengine walianza kutunga mashairi kwa kuasi kaida na desturi zilizozoeleka (arudhi). Hili linabainika katika diwani kama vile *Kichomi*.

Kuhusu lengo la tatu, utafiti ulionyesha changamoto zilizotokana na mitindo na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi. Matokeo yalionyesha kuwa upya katika uwasilishaji wa mpangilio wa mistari, maneno na upwa wa vibwagizo katika *Tunu ya Ushairi* unazua changamoto kwa wahakiki wa mashairi katika kufasili istilahi zilizozoeleka. Kwamba, kuna ruwaza tofauti na zile ruwaza za awali za kutunga mashairi kwa kuzingatia vipengele vilivyotajwa.

Kujumuishwa pamoja mashairi mbalimbali, kunasaidia kuondoa mipaka iliyokuwepo awali iliyotenganisha ushairi arudhi na ushairi huru. Upya katika kuwasilisha ushairi arudhi katika bahari zake pia ni hatua inayozua changamoto katika namna ya kufasili dhana mbalimbali ikiwemo dhana ya ngojera. Kwa hivyo, changamoto zinatokana na ufasili wa dhana na maana za kishairi katika muktadha wa awali wa hali zilizozoeleka. Utafiti ulibainisha ya kwamba nadharia ya mtindo ni muhimu katika kuchanganua mtindo wa kazi fulani. Hii ni kwa sababu, kazi za kifasihi haziwezi kubainika bila kuzingatia namna zilivyosawiriwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia ujumbe husika.

#### **5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ulijishughulisha na changamoto zinazotokana na mikondo na mitindo mipya ambayo watunzi wa mashairi wameibuka nayo sasa. Utafiti umebainisha kuwa, kuna haja ya kupanuliwa na kubadilishwa kwa istilahi zilizozoeleka kuhusiana na ushairi ili kuendana na hali ya sasa ya maendeleo ya utunzi. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu kutatua changamoto zilizozobainishwa kwa kupanua istilahi zilizozoeleka na kubadilisha zile mbazo haziafikiani na hali ya sasa ya utunzi. Utafiti zaidi pia ufanywe kuhusu manufaa yatokanayo na ujumuishwaji pamoja wa mikondo na mitindo mbalimbali ya utunzi wa mashairi katika diwani moja.

### Marejeleo

- Abedi, A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri*. Kenya Literature Bureau, Nairobi
- Allen, G. (2000). *Intertextuality*: New York. Routledge 29 West 35<sup>th</sup> Street.
- Arege T. (2013). *Tunu ya Ushairi*. Oxford University Press, East Africa Ltd: Nairobi.
- Babusa O. (2005). *Vigezo badilia kuhusu uanishaji wa mashairi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapiswa).
- Bakhtin M. (1981). *Theory of the Text*. London: Routledge.
- Chacha, M. (1987). *The Meaning and Interpretation of Swahili Poetry*. Ph.D Thesis. Yale University.
- Coombs, H. (1953). *Literature and Criticism*. London. Chatto and Windus.
- Gakuo, J. (1996). *Fani katika Utenzi wa Vita vya Uhuru*. Tasnifu ya M.Phil, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa)
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Education Books.
- Kezilahabi, E. (1982). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- King'ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: G U P
- Masinde, E. (2003). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui*. Tasnifu ya Ph.D. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Masinde, E. (1992). *Mitindo katika Mashairi Huru*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).



- Momanyi, C. (1991). *Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dares Salaam. Tanzania Publishing House.
- Nabhany, A. (U.D) *Swahili poetry and prosody*.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia ya Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyanchama, M. (2004). *Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhidi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).
- Robert, S. (1972). *Sanaa ya Ushairi*. Nairobi: Thomas, Nelson and Sons.
- Senkoro, F. (1988). *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam.
- Walah, W. (1988) *Malenga wa Ziwa Kuu*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Misingi ya Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- Wafula, R. (1992) *Mawazo na Mbinu alizotumia Chacha katika Tamthilia ya Marejeleo*. Katika mwamko toleo la tano.

## VIAMBATISHO VYA MASHAIRI YALIYOTUMIWA

### VIDATO VYA MAISHA (Ukurasa wa 59)

Vidato  
vya  
maisha

Mithili

ya  
sarafu;

kipo  
kichwa

nao  
wa  
pili  
upande.

Kuna  
kupanda

na  
kushuka,  
kupenda

na  
kuchukia,

kufaulu

na  
kushindwa.

Leo  
utapanda,

kesho  
washuka.

Ni  
kawaida

ya  
maisha;

mdundo

wa  
moyo,

burdani

ya  
nafsi!

**Bwana na Mke (Ukurasa wa 36)**

Bwana: U hali gani azizi?                      Mke: Hali yangu njema Bwana  
 Bwana: Khabari za matembezi?              Mke: Kwa kweli salama sana  
 Bwana: Wa'hali gani wazazi?                Mke: Wote wazima kibwana

Wote: Twashukuru kukutana, sisi wapenzi wawili  
 Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali.

Bwana: Ilikuwaje safari?                      Mke: Bwana nashindwa kunena  
 Bwana: Ilikuwa ya hatari?                    Mke: Hapana Bwana hapana  
 Bwana: Ilikwenda vizuri?                    Mke: Kama unavyoniona

Wote: Twashukuru kukutana, sisi wapenzi wawili  
 Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali.

Bwana: Nakuona wapendeza                Mke: Na wewe ninakuona  
 Bwana: Bali wewe wang'ariza,              Mke: Wewe mwezi wafanana  
 Bwana: Afya haukupoteza,                 Mke: Na wewe waonekana

Wote: Twafurahi kukutana, sisi wapenzi wawili  
 Tangu tulipotengana, kwa kuishi mbalimbali.

Bwana: Hapa ninapumzika                    Mke: Nami la kusema sina  
 Bwana: Natumuombe Rabuka,                Mke: Ndiye Yeye Subuhana  
 Bwana: Atupe zake baraka                    Mke: Maisha yetu kufana

Wote: Twafurahi kukutana, sisi wapenzi wawili  
 Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali.

Baraka na Ali (Ukurasa wa 73)

B: Hodi hodi bwana Ali, hodi ndani samahani!

A: Karibia tafadhali, karibu ingia ndani.

B: Nakushukuru kikweli, kwa karibu ya hisani.

A: Umetoka huko mbali, azma yako ni nini?

B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.

A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.

B: Tunamshukuru sana, kwa mapenzi ya moyoni.

A: Tabia ya kuonana, si leo tangu zamani.

B: Ni kweli unayonena, hayapati ukinzani.

A: Ama watu kupendana, humpendeza Manani.

B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.

A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.

B: Lakini Bwana Bakari, habari gani shambani?

A: Kuna mavuno mazuri, kwa chakula cha mwakani.

B: Na sisi kwetu tayari, mavuno yamo ghalani.

A: Neema jambo la kheri, nchi huwa furahani.

B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.

A: Twamshukuru Manani, shaka yetu huko kwenu.

B: Haya sasa tuagane, tuagane kwa kherini.

A: Na tuombe tuonane, kwa afya njema mwilini.

B: Na tuombe tushikane, kama pete kidoleni.

A: Kwa mema tuhimizane, ndugu na zetu jirani.

B: Nimekuja waoneni, na kujua hali zenu.

A: Twamshukuru Manani, shaka ni nyumbani kwenu.

**Nilikupa Ukatupa (Ukurasa wa 77)**

Nilikupa, kila changu, ukatupa

Nilikupa, dhati yangu, ukatupa

Nilikupa, moyo wangu, ukatupa

Nilikupa, siri yangu, ukatupa

Nilikupa, kweli yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa

Nilikupa, roho yangu, ukatupa

Nilikupa, wema wangu, ukatupa

Nilikupa, mwili wangu, ukatupa

Nilikupa, ngeu yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa

Nilikupa, chembe yangu, ukatupa

Nilikupa, utu wangu, ukatupa

Nilikupa, hadhi yangu, ukatupa

Nilikupa, jina langu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa

Nilikupa, tabu zangu, ukatupa

Nilikupa, raha zangu, ukatupa

Nilikupa, sera yangu, ukatupa

Nilikupa, ghera yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa, cheko zangu, ukatupa  
 Nilikupa, chozi langu, ukatupa  
 Nilikupa, njozi langu, ukatupa  
 Nilikupa, sihi zangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa, nuru yangu, ukatupa  
 Nilikupa, dira yangu, ukatupa  
 Nilikupa, asa yangu, ukatupa  
 Nilikupa, nira yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa, uso wangu, ukatupa  
 Nilikupa, nguvu zangu, ukatupa  
 Nilikupa, jicho langu, ukatupa  
 Nilikupa, ngome yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa, sifa zangu, ukatupa  
 Nilikupa, sudi yangu, ukatupa  
 Nilikupa, suna yangu, ukatupa  
 Nilikupa, kufu yangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa, kiu yangu, ukatupa  
 Nilikupa, hisi zangu, ukatupa  
 Nilikupa, radhi yangu, ukatupa  
 Nilikupa, nyonda zangu, ukatupa.

Nilikupa, kila changu, ukatupa  
 Nilikupa maisha'ngu, ukatupa  
 Nilikupa, mafa yangu, ukatupa  
 Nilikupa, sanda yangu, ukatupa  
 Nilikupa, kasha langu, ukatupa.

**Siondoki (Ukurasa wa 87)**

Eti

Niondoke!

Mimi niondoke hapa

Niondoke hapa kwangu!

Nimesaki; licha ya risasi

Vitisho na mauaji, siondoki.

Mimi

Siondoki

Siondoki siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Kwa mateke hata na mikuki

Marungu na bunduki, siondoki.

Hapa

Siondoki

Mimi ni pahame!

Niondoke hapa kwangu!

Fujo na ghasia zikizuka

Na kani ya waporaji, siondoki.

Haki

Siondoki

Kwangu siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Nawaje; waje wanaokuja

Mabepari wadhalimu, siondoki.

Kamwe

Siondoki

Ng'oo hapa kwangu!

Katizame chini mti ule!

Walizikwa babu zangu, siondoki.

Sendi

Nende wapi?

Si'hapa kitovu changu!

Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi

Si kwamba hapa si kwangu, siondoki.

Katu

Siondoki

Sihitaji karatasi

Niondoke hapa kwangu

Yangu mimi ni ardhi hii

Wala si makaratasi, siondoki.



**Lauzi, Mwanangu (Ukurasa wa 89)**

Ewe mwanangu Lauzi, Lauzi binti yangu  
 Zidariza beti hizi, hizi wasia wangu  
 Ukuapo umaizi, umaizi ulimwengu  
 Kwamba hauna mjuzi, mjuzi wa ulimwengu  
 Hajawapo pande hizi, hizi toka babu zangu  
 Tangu kuwepo Wangozi, Wangozi hata Wazungu  
 Kila aliye ajizi, ajizi yake ni pingu  
 Kisha hulewa ulezi, ulezi wa ulimwengu  
 Usokuwa na mbawazi, mbawazi ila machungu  
 Yasikufike mwanangu, mwanangu nakuusia.

Mwanangu nakuusia, nakuusia Lauzi  
 Chuo kigumu dunia, dunia hii kozi  
 Huwezi mia kwa mia, mia kufuzu huwezi  
 Utaishia kulia, kulia pasipo chozi  
 Muradi ukijitia, ukijitia bazazi  
 Kikiki kushikilia, kushikilia ushenzi  
 Tarudi kuujutia, kuujutia upuzi  
 Dunia kikukalia, lia kutoka huwezi  
 Ewe mwanangu ridhia, ridhia haya malezi  
 Yenye na kila mbawazi, mbawazi na maongozi.

Mbawazi na maongozi, maongozi mema kwako  
 Mama sichelee kazi, kazi ni wajibu wako  
 Siwe mwana mlegezi, mlegezi hana meko  
 Ungapenda kubarizi, kubarizi na wenzako  
 Kushiriki simulizi, simulizi na vicheko  
 Na hiari sikatazi, sikatazi haki yako

Lakini nawe maizi, maize msada wako  
 Kusaidia wazazi, wazazi hasa mamako  
 Japo kwa kukuna nazi, lako tenda kwa hiari.

Lako tenda kwa hiari, hiari bila chukizi  
 Mukhtari uwe mori, mori wa kutenda kazi  
 Iwapo siku ujiri, ujiri kuwa mzazi  
 Hapo wako umahiri, umahiri wa kikazi  
 Hudhihirisha athari, athari za kimalezi  
 Hudhihirika dhahiri, dhahiri zikawa wazi  
 Ikawa kutahayuri, kutahayuri ushenzi  
 Ndiposa nakushauri, nakushauri Lauzi  
 Ulegezi usibiri, usibiri ulegezi  
 Siafiki ubazazi, ubazazi ni chukizi.

Ubazazi ni chukizi, chukizi kwetu wakera  
 Siyo ghere ya mlezi, mlezi mwenye busara  
 Hawi dira ya matenzi, matenzi yenye madhara  
 Yapayo mwana ukazi, ukazi wa mbaya sera  
 Akawapora wakazi, wakazi wenye mapora  
 Kupora ng'ombe na mbuzi, mbuzi hata biashara  
 Kuna siku ya Mwenyezi, Mwenyezi mwenye kudura  
 Madhara ya virumbizi, vizumbizi na bakora  
 Yamzidipo ni wazi, ni wazi roho hugura  
 Usambe mwana wakora, wakora wanauawa.

**Waite (Ukurasa wa 99)**

Waite, walio mbali, muufanye ushirika  
 Waite, japo wawili, wao nao kuhusika  
 Waite, wengi ni mali, mmoja wachacharika  
 Waite, wengi sahali, mmoja utaanguka  
 Waite! Wengi waite!

Waite, ujenge nguvu, mufanye nyote pamoja  
 Waite, siwe mvivu, huwa ni nguvu umoja  
 Waite, wasaidivu, pekeyo watakupija  
 Waite, muwe ja ndovu, muwakanyage mapaja  
 Waite! Ndugu waite!

Waite, wache tengano, utengano udhaifu  
 Waite, kwa mapambano, usipatwe na hawafu  
 Waite, wambe maneno, muupiku udhaifu  
 Waite, muume meno, ili kuushinda ufu  
 Waite! Ndugu waite!

Waite, muwache woga, mzikomeshe dhuluma  
 Waite, bila kurega, ndimi zenu kuungana  
 Waite, vaa daluga, mshikane kulalama  
 Waite, mwende kupigana, ukombozi kuuchuma  
 Waite! Ndugu waite!

**Monyara (Ukurasa wa 101)**

Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara  
 Tuliochelea kukaribia kingo zake  
 Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia

Kwa kunyenyekea wingi wa yake maji  
Yaliyojiendea utadhani yamesimama.

Ni katika mto huu  
Ambapo samaki wakubwa tulivua  
Maguo kuyatakasa japo kwa kuunyemelea  
Na walevi stadi wakachelea kuuvuka  
Ulipo fura na kupita kwa kiburi  
Kwa kushiba maji yake  
Yaliyofanya mawimbi madogo.

Ni hapa ambapo marehemu nyanya  
Mkono alinishika na njia kuniongoza  
Juu la ulalo wa miti  
Vikapu vyetu hewani vikielea;  
Mimi nikishika changu kwa mkono mmoja  
Naye akikiachilia chake kujishikisha kichwani  
Masafa baina yetu na mtambo  
Uliokwenda kwa nguvu za maji  
Tuliyapunguza kwa kila hatua tulopiga.

Ni katika mto huu ambapo  
Samaki tuliowavua tuliwapasua na kuwasafisha  
Na hivyo kuuficha umaskini wetu  
Ulotuzuia kununua mnofu wa bucha  
Ni hapa ambapo wanawake walifika  
Mawe ya kusagia kupata  
Ni katika mto huu ambapo  
Waumini walifika kutakaswa kwa ubatizo

Baada ya ulevi, uzinzi na kufuru nyinginezo.

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa  
 Hata wachawi walifika kufanya vitimbi vyao  
 Baada ya utawala wa jua kumezwa na nguvu za giza  
 Sasa Monyara niloijua haipo tena  
 Zimebaki kingo zilizokaukiana  
 Kama uso wa mrembo aliyekosa mafuta  
 Siku ayami.

Mto huu ambapo pembeni mwake  
 Watoto walipashwa tohara  
 Maji yake yakishangilia, umekonda  
 Na mbavu zake nje kutoa  
 Na sasa vitoto vikembe vinazikanyaga  
 Vikijiendea zao kusaga mahindi  
 Juu mlimani  
 Katika mtambo wa Kizungu  
 Usioisha kulalamika  
 Nao wanawake hawaji tena  
 Kutafuta mawe ya kusagia wimbi  
 Imebaki njia ya walevi warejeao nyumbani  
 Nayo miti iliyosimama wima ukingoni  
 Iliisha kuanguka kwa kuleweshwa na pumzi za walevi  
 Wasioisha kupita hapa.

**Sina Hakika! (Ukurasa wa 109)**

Mimi tena sina tofauti  
 Na chumvi iliyoguswa na maji;

Ukali umo kasoro udhahiri.

Mlima wakodoa macho mbele yangu  
Kiini cha ngoma kinazidisha mlio  
Natulia na kujisaili.

Natambua u pale pale  
Unanitizama  
Unanihimiza kimya kimya  
Nahisi unanidara  
Lakini  
Sina hakika!

Upeo wake umeongezeka maradufu  
Katika kiini cha damu na fikra zangu  
Ninapiga hatua  
Kila mguu wauhimiza mwenziwe kuanza  
Naona kama yote inasonga  
Wakati huo huo inasita  
Kama kuuomba moyo idhini!

Moyo unachekeka sawia na mlima  
Nasikia maneno fulani  
Sina hakika ni sauti ama fikra:  
Ni kanuni hii  
Mimi bado nipo  
Siku zote ulinikanyaga  
Na uso kuniparuza  
Wala sikulalamika

Mwenyewe utakapochoka usihofu  
 Tumboni nitakusetiri  
 Lakini kwa sasa tamba  
 Japo kwa kuogopa  
 Hii awamu ya lala salama!

**Pendo la Pesa (Ukurasa wa 116)**

Pendo la pesa si pendo, mbali nalo jitengee  
 Pendo lanuka uvundo, mbali nalo lisogee  
 Pendo halina uhondo, katu usilichekee  
 Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo halina utamu, lina harufu jamee  
 Pendo ninalilaumu, mimi lisiinilemee  
 Pendo halina kudumu, hadi pesa umwekee  
 Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo lataka kupenda, bila kupiga kengee  
 Pendo mfano wa tunda, ukila unenepee  
 Pendo la pesa huvyonda, tupa usilipokee  
 Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo la kwa kila hali, ubora nalipotee  
 Pendo kutumia mali, ndipo aitike bee  
 Pendo hilo ni dhalili, mbali nalitokomee  
 Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo kutumia hela, mifuko iteketee  
 Pendo hilo lahaula, ni zigo ujibebee,

Pendo wawili ni kula, nyama ndimi mnenee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo kwa watu chaguo, lazima nielezee  
Pendo ni sawa funguo, kufuli imngojee  
Pendo la kupenda nguo, bora lichekwe heehee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo ni la pale zama, wanahadithi wazee  
Pendo lao likiuma, bila kusema nige  
Pendo sasa limelema, ukipanda lisimee  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

Pendo hapa nakomesha, mbele nisiendele  
Pendo la pesa lafisha, ni gonjwa usipokee  
Pendo hadhi linafisha, la pesa sipendele  
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.

### **Siku Zimesonga (Ukurasa wa 123)**

Ulikuwa utarudi!  
Sikudhani ungerudi, mahaba yalivyokonga  
Kusubiri ingebidi, ela siku zimesonga  
Nilibaki sina budi, ila mlango kufunga.

Ulikuwa utarudi!  
Nilidhani kafaidi, huko ulikwenda tanga  
Japo endaye hurudi, ela siku zimesonga  
Mpendwao mna kedi, hamuishi kujiringa.



Ulikuwa utarudi!  
 Moyo ulitaradadi, kasha ukatia nanga  
 Ninasikia hodi, ela siku zimesonga  
 Wanamba wangu fuadi, huba limesha jitenga.

Ulikuwa utarudi!  
 Kuwepo kwako baidi, majuto yalinizonga  
 Na ingawa umerudi, ela siku zimesonga  
 Pendo sipi mkaidi, japo nikatwe mapanga.

**Vifusi vya Damu (Ukurasa wa 125)**

Njiwa waliokuwa juu wakiruka  
 Na mapaani kwetu kutua  
 Kotekote wakafurika  
 Na yao mvumo kukolea  
 Sasa wameadimika  
 Wakabaki kuhadithia.  
 Imebaki sasa mikoromo  
 Ya zao tingatinga  
 Pamoja na mingurumo  
 Ya ndege zao zinotanga  
 Zisizoisha mifumo  
 Ya uhai kuunyonga.

Vimebaki vifusi  
 Chini ya mahame haya  
 Wamezikwa ndugu zetu  
 Walioachwa kujiozea  
 Chini ya magofu.

Yamesalia siyo matuta ya mchanga  
 Tuliyozea kucheza mwajificho  
 Bali vichuguu visivyo kikomo  
 Vilivyochanganyika na damu  
 Ya jamaa zangu  
 Ambayo ilishikanisha pamoja  
 Mchanga uliovijenga vichuguu vipya  
 Vilivyojaliwa baada ya mngurumo mkubwa kusikika  
 Ndani mwake mna mifupa; vyuma vya kukiimarisha  
 Kichuguu hiki ambacho nachelea kukikaribia.  
 Sasa limebaki kutanda wingu zito jeusi  
 Nami kompyuta yangu ya mawazo  
 Hamasisho ipatapo  
 Machozi hunitoka taratibu  
 Kama bomba la maji lililotoboka.

Machozi yasiyoweza kuwarudisha tena  
 Wale njiwa weupe  
 Walioimba nyimbo bembelezi.

Machozi haya yazamapo chini mchangani  
 Najua mchanga uliochanganyika na damu  
 Yanaufikia na kichuguu kukiimarisha  
 Hadi mchwa chini watakapotoka  
 Na chao kichuguu kukijenga  
 Kwa yao mate.

Ingawa bado mavumbi yatifuliwa  
 Kwa yao makombora

Najua siku moja itanyesha  
 Kubwa mvua ya kulinyonga vumbi  
 Ili njiwa wapate kuiona tena njia  
 Ya kuwarejesha mara nyingine  
 Hapa Mashariki ya Kati  
 Ambapo mtoto huyu mchanga  
 Anaendelea titi kulinyonya  
 La mamake aliyelala usingizi usio mashaka;  
 Baada ya kushindwa kucheza mwajificho  
 Na makombora katika msokotano  
 Wa hivi vilima vilivyojengwa kwa mifumo.

**Rai na Mawaidha (Ukurasa wa 129)**

Umbea kasema babu, umbea magaragaza  
 Umbea ukihutubu, umbea takufukuza  
 Umbea si matulubu, umbea utateleza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea unaharibu, umbea si kupendeza  
 Umbea si mahisabu, umbea katu kujaza  
 Umbea ni majisibu, umbea unapunguza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea ujishurubu, umbea kuukataza  
 Umbea tujitanibu, umbea mbali kusoza  
 Umbea si njema gubu, umbea huna mwangaza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea sawa shahabu, umbea si majikweza  
 Umbea ai! Ghayubu, umbea si kiambaza  
 Umbea huna thawabu, umbea hujajipoza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea mwenye vitabu, umbea umekataza  
 Umbea Bwana Wahabu, umbea hakuongoza  
 Umbea ukijaribu, umbea takuunguza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea kheri ya tabu, umbea kwa mbaya jaza  
 Umbea wote tutubu, umbea tuloparaza  
 Umbea sio jawabu, umbea jama zazaza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.  
 Umbea mbaya adabu, umbeya si matukuza  
 Umbea mbaya kulabu, umbea katu kukaza  
 Umbea si unaibu, umbea hukandamiza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

Umbea tama twaibu, umbea ninamaliza  
 Umbea magabugabu, umbea wacha kuwaza  
 Umbea tuupe tibu, umbea kuugombeza  
 Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.

**Ndumilakuwili (Ukurusa 146)**

Mbona waleta utata  
 Wa mambo kuyavuruga?  
 Mbona huishi papara  
 Na nyingi

a k  
 l u  
 I w  
 m i  
 u l  
 d i  
 n ?

Keti, tulia, makinika, tafakari

Sote tuketi chini hapa

Chini ya hili letu jengo

Pamoja tufanye shirika

Shirika la shikamano

Kabla giza kutanda.

### **Maisha Vidato (Ukurasa wa 159)**

Maisha yana vidato

Si viwili si vitatu  
 Hayana njia mkato  
 Kama watakavyo watu  
 Mja kienda endato  
 Sije kapata sepetu.

Siendi kama kipofu  
 Asejua aendako  
 Nenda kwa uangalifu  
 Makini na hamasiko  
 Ingawa ni ndefu njia  
 Utafika uendako.

Kuna kwingi kuinuka  
 Kisha kuna tambarare  
 Na pia kuteremka  
 Hamrere hamrere  
 Kaa ukiyakumbuka  
 Dunia si nguo sare.

**Vipande Viwili (Ukurasa wa 160)**

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Ni mengi yamenifika, mradi kunithakili  
 Nusura niwe mahoka, kwa vurugu la akili  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Kila saa na dakika, asubuhi na laili  
 Roho yanipapatika, sikai wala silali  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Mno nimehangaika, kamwe sijatua tuli  
 Mwili umedhoofika, na ubongo na akili  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Mwili nimeatilika, nimeatilika mwili  
 Hivi nimedhalilika, kwa wingi wa idhilali  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Nishikalo la ponyoka, sawa na pepo za vuli  
 Ulimwengu wanicheka, ninapaliwa kejeli  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Nimeandika nyaraka, Zaidi ya mara mbili  
 Kumuomba muhibaka, turudi kuwa wawili

Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Rai zilipomwagika, kutaka yake kauli  
 Neno halikumtoka, japo kwa kunikejeli  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Nimezengea viraka, na uzi wa silisili  
 Ila bado natabika, sijapata afadhali  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Moyo umehamanika, kuniepuka halili  
 Japo nimewajibika, kusihi hanikubali  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

Tangu liliporaruka, huba vipande viwili  
 Inakaribia mwaka, na usingizi silali  
 Niombeeni Rabuka, iboreke yangu hali  
 Nimebakia hamali, moyo hukunisaili.

**Ni Makini (Ukurusa wa)**

Ulinikataa,	tangia zamani
Ukaniambaa,	mwangu ubavuni
Na nyingi shufaa,	zangu samahani
Hazikunifaa,	hukuzithamini
Nilikushangaa,	kwa wako uneni
Nikakakamaa,	kwa wingi huzuni
Ziliponivaa,	sikujithamini
Lakini jamaa,	watu wa nyumbani
Hawakuzubaa,	kuja niauni
Hivi zimepwaa,	dhiki na huzuni.

Hivi nimekaa  
Tuli ni makini  
Sijakukataa  
Lakini! Lakini!  
Kulia nyamaa  
Nilikuthamini  
Ukanikataa  
Ul'owathamini  
'Waje kukutwaa  
Mimi samahani.

Mahaba kupaa,	ni tangu zamani
Kwa as'oyatwaa,	akayathamini
Huja akakaa,	chanda mdomoni
Uligaagaa	nikiwa pembeni
Sichi kushangaa,	wala kukuthamini
Ninga kukataa,	wajuwa kwa nini
Bikira kuzaa,	ingawa ni soni
Hawakushangaa,	kina Firauni
Hivyo taataa,	pole sikudhani
Ingezima taa,	kwako kisogoni.



**Subira na Imani (Ukurasa wa 171)**

Mungu naomba subira, subira nayo imani  
 Imani iliyo bora, bora hapa duniani  
 Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani  
 Hiani pamwe ukora, ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhuli  
 Ufidhuli wa kudhuri, kudhiri wangu muwili  
 Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili  
 Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele  
 Muwele wa hitilafu, hitilafu ya nduwele  
 Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele  
 Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vinitomele vikwato  
 Vikwato pia maole, maole kufanya mito  
 Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto  
 Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fukuto.

Fukuto lanipa neon, neon hili kutamka  
 Kutamka wazi vino, vino subira kutaka  
 Kutaka Imani mno, mno n'sipate wahaka  
 Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita  
 Yamepita na vilio, vilio vipishe nyota  
 Nyota njema ing'arao, ing'arao kunikita

Kunikita salamani, salamani nikadata.

**BURIANI(Ukurusa wa 54)**

Ndugu aliye muhibu,kaaga nenda mjini  
 Nikasake ya wajibu, na kutia jicho shani  
 Takayefika mjibu, sendi kawia mjini  
 Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa

Kituoni alingoja, usafiri ni wajibu  
 Mara gari hilo laja, kaingia bila tabu  
 Kumbe vile ni mauja, yangoja wetu muhibu  
 Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa

Dereva kawa kituko, kaendesha kwa mikogo  
 Sukani huku na huko, kauvuta kama gogo  
 Kichwa chake sawa kuko, kajaza pombe ni zigo  
 Buriani ndugu yangu, kuonana majaliwa.....

**Tamadunizo Siase (Ukurusa 51)**

Dada Umbu hayo ni kusudi, au ndiyo miujiza?  
 Nakuona meshitadi, kulia jambo waigiza,  
 Ndipo kawa sina budi, leo kweli kukujuza,  
 Usije kajipoteza, tamadunizo kuasa

Dada kaka hela tabarudi, moto wako kupunguza,  
 Naona wataradadi ukuhani kujikweza,  
 Ni wako upi muradi, utakao kunijuza?  
 Nambie naloigiza, ni utamaduni gani?

Kaka Mbona waja kali sasa, name nakuelekeza?  
 Tuongee kisiasa, hai mana kuchagiza  
 Kuigiza ndicho kiza, khususa kizungumza,  
 Wajifanya Mngereza, ni utamaduni gani?

Dada Kaka wafanya makosa, kisema nimeigiza  
 Sababu metowa pesa, lugha hii kujifunza  
 Mejifunza kwa mikasa, kichapwa nikijikaza,  
 Hela nalouigiza, ni utamaduni gani?

Kaka Kuwa umeilipa, ni kweli sekukataza,  
 Si vimbi ukitumia, kazi unakofanyiza,  
 Ela we na Fauzia, vipi mwamba Kiingereza?  
 Bali wajitendekeza, tamadunizo kuasa.

Dada Si mimi kuningilia, nawe pia waigiza.  
 Kishapo watufanyia, mengi yanayochukiza,  
 Kama bangi kuzitia, ni dawa yani neleza?  
 Akili kuitatiza, ni utamaduni gani?

Kaka Dadangu bangi si sumu, ya mtu kumuumiza,  
 Kamwe haina wazimu, kama unavyoiwaza,  
 Bali yakwe masitimu, mawazo huyapunguza  
 Ela we umeongeza, tamadunizo kuasa

Dada Nambia kweli umbulo, kwani nishapeleleza,  
 Kija nyumbani kwa mlo, hutaki kuzungumza  
 Walibugia bofulo, mpaka kutushangaza,  
 Kisa ni bangi neleza, ni utamaduni gani?

Na kisha wanishitumu, ati ati naigiza  
 Hela ituze fahamu, sijione wapendeza,  
 kuvaa beli-botomu, makaio kuyakaza,  
 We mwenyewe peleleza, ni utamaduni gani?

Kaka Kweli nakueleza, usifikiri nacheza,  
 Beli walotuletea, ni wahenga waloanza,  
 Lakini zenu 'flea', mwawaiga wangereza,  
 Sijitie makengeza, tamadunizo kuasa.

Dada Sitokoma jitetea, kinizulia taiza,  
 Hivyo nitaendelea, hadi tutakaposoza,  
 Bilashi wanionea, hali najiendeleza,  
 Pasi kujiendeleza, ni utamaduni gani?

Kaka Dada hatuoneani, bali nakuelekeza,  
 Kwani mwenyewe huoni, kuna mambo yachukiza,  
 Viguo vya mapajani, sidhani vyakupendeza,  
 Bali ni kuhinikiza, tamadunizo kuasa.

Dada Miniikati ni nin? huvaa anaeweza,  
 Ni nguo za nisiwani; wenye viga hupendeza,  
 Ela we haya huoni, mke ukimuigiza?  
 Mikufu wajifungiza, ni utamaduni gani?

Kaka Hata nami huchukia, mume mkufu kukaza,  
 Lakini kiangalia, hilo si la kuchukiza,  
 Kama nyele za bandia, mnazojibandikiza,

Nyelelezo wazipuuza, tamadunizo kuasa.

Dada Nami silipendi pia, kuvaa nyele uoza,  
 Za asili naridhia, alizonipa muweza,  
 Ela viatu udhia, Santana vyashangaza,  
 Wachenda wana mikogo, ja walouguwa funza,  
 Mtu wajiendekeza, tamadunizo kuasa.

Kaka Twalonena si kidogo, mengi tumezungumza,  
 Tujipunguze miigo, kuiga yasopendeza,  
 Asili kuipa sogo, utumwa twajfungiza,  
 Twige ya kutuongoza, kwenye tamaduni zetu.

**Panda (Ukurasa wa 44)**

Panda, panda la mnazi, l'anzalo kupapatuwa  
 Panda juu ya malezi, moyo wako wishe ngowa  
 Panda mti wa mapenzi, uwepushie na juwa  
 Panda ni wako uluwa.Panda darajari, Panda!

Panda juu ya farasi, kwa haiba na sitawa  
 Panda kiwango mkwasi, uukimbie ukiwa  
 Panda, situpe viasi, wendako ukikujuwa  
 Panda, ni wako uluwa.Panda darajani, Panda!

Panda ngano na mpunga, afudhali ya viliwa  
 Panda wimbi na kimanga, vipawa vya wa kupewa  
 Panda, usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa  
 Panda ni wako uluwa. Panda darajani, panda!

Panda mwema mshajari, wite t'anzu na mauwa,  
Panda utunde johari, mwivi asijezanguwa  
Panda juu ya mimbari, ulingane sawasawa  
Panda ni wako uluwa. Panda darajani, panda!